# Fasheni yenye afya



Mwandishi: Grace Momadi-Masaka -2012, Arusha, Tanzania

Cover: Sharon Ondieki-Nairobi-Kenya

MaarifaMtandaoni.com | RohoYaUnabii.Org

MAGONJWA YA MITINDO NA ATHARI ZAKE

## Utangulizi

Napenda Kumshuru Mwenyezi Mungu kuhusu makala hii niliyoandika mwaka 2012, na hili ni tolea la pili. Napenda kuwashukuru matatibu Clifford Majani na Dorcas Ayayo, kwa madarasa na notes nilizochukua kutoka kwao. Hawa wamefundisha masomo haya na hata kuandika vitabu. Tunakualika utuandikie na kutupa mashauri kuhusu mada hii na mada zingine.

Habari ambazo zinaendelea kuvua mitandaoni ni nyingi (trending) na watu hupenda kuyaigiza, hebu tuwe na busara na kichujio katika yote! Watu wana upweke na ombwe/tupu wa aina fulani hivyo hufanya mambo fulani ili kujisikia furaha. Hakika furaha ya kweli ni ile Mungu alituumbia ndani ya mioyo yetu wanadamu. Nilisoma kwamba kuna mtu Japani alipenda mbwa sana na kushona suti ili awe kama mbwa anayetembea barabarani. Alitumia dola 15,000 kuishona suti hii na kutembea barabarani ili kuwaonyesha watu! Hizi ni kama shilingi arobaini milioni za Tanzania.

Twapaswa kujiuliza mara nyingi kwamba mimi ni nani, nipo hapa duniani kwaajili gani na naelekea wapi. Kila mwanadamu anapendwa sana na Muumba Wake, hata hahitaji kufikiria anahitaji kuwa na kitu fulani au kuvaa hivi na vile, ili akubalike, hii ni hekima ambayo Muumba anawapa wananadamu wote kila siku, kwani kuna utupu mioyoni mwetu hadi tuishi kile ambacho tuliumbiwa. Msukumo wa ombwe sio suala la kijamii pekee yake, bali ni suala la kiroho, Mfalme Sulemani alisema “ Nimezona kazi zote zifanywazo chini ya jua, na tazama zote ni ubatili na kujilisha upepo”. Kujilisha upepo ni hali ya nafsi kutafuta kutoshelezwa na vitu visivyoweza kuuridhisha moyo, na hivyo tunaendelea kutafuta vingine zaidi!

Sisi wanadamu ni sehemu tu ya Uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Yeye hutuamsha na kutusaidia na kutuletea furaha ya kudumu, Yeye ametuumba kwa namna ya pekee, nasi mioyo yetu haina utulivu, hadi itulie ndani Yake tu. Tunaweza kumuita  hata kabla hatujamjua kabisa! Yeye atatupa malengo na maana ya maisha yetu, na kutupa balansi/uwiano mzuri, kwamba hatuendi mbele sana kwenye mambo ya fasheni, na wakati huo huo hatupo nyuma sana na hivyo kuonekana kituko fulani mtaani! Mwisho wa makala haya mengi yameandikwa ya kutusaidia safarini. Hebu lile ombwe au utupu wa moyo, tulijaze na Ahadi Zake Bwana alizozitamka ambazo ni maelfu.




Yaonekana watu wengi na hasa sisi wanawake tunapenda mambo ya mitindo na kujipamba pia. Shida hizi ni za toka enzi za mababu, hakuna jipya chini ya jua; wakati wa Wamisri, na Wababeli pia. Toka mama yetu Hawa alipotaka aonekane tofauti kwa kujua mengi pale bustanini, mambo mengi yametukumba. Alitaka kufanana na Mungu, na tayari alikuwa kiumbe pekee aliyefanana na Mungu. Sote tuna shida, ni kitu cha kuombea kila siku. Kuwa maridadi ni kitu kizuri ila kupoteza afya au kukosa adabu sio jambo zuri. Tutajuaje tunapotoka nje ya mstari, na watu wa kileo/kisasa huwa hawamwambii mtu bali wanamsengenya? Ni kweli tusivae magunia, ila kama unataka watu wakutazame sana, basi magunia ndiyo yanafaa, maana kwa mitumba na utandawazi uliokuja, nguo nzuri zimezagaa kila mahali. Hakuna mtu asiyetaka kupendeza au kuonekana, ila kutunza afya ni muhimu pia.

Watoto wetu wakiona tumevaa vitu vya ajabu, wanatuiga na kuongeza mabaya zaidi. Tukivaa nguo fupi hadi mpaka magotini, wao watavaa fupi hadi mapajani. Tukiacha kifua nje, wao wataacha matiti nje. Ni jambo la mtu binafsi kuombea na mambo ya viatu, mavazi, a na mapambo ya mwili.

Soma katika Wimbo ulio Bora wa Mfalme Sulemani na nabii Isaya kuhusu mapambo, Njuga, wanja, vioo, mikanda na vinginevyo. Hivi sio vigeni kwani vina zaidi ya miaka 5000. Kwa vile makala haya yatazungumzia kuwa makini na mitindo isiyoenda na afya hivyo tutazungumza kidogo tu kuhusu fasheni, kwasababu hata hivyo fasheni hupita nasi pia hatujui upo nchi gani na fasheni huko ni nini, maana fasheni zinaenda mbele na kurudi nyuma. Tumeona mitindo mingi inayoharibu afya iwe ni kuweka nywele katika kope za machoni ili zionekane refu (eyelashes), iwe ni kuvaa viatu virefu nk

“Bwana Akasema tena, kwa sababu binti za Sayuni wana kiburi, na kuenenda kwa shingo zilizonyoshwa, na macho ya kutamani, wakienenda kwa hatua za madaha, na kuliza njuga kwa miguu yao.” Sura hii imeonyesha vitu vingi vya mapambo ambayo ni vya miaka zaidi ya miaka 2500! Hapa kuna mapambo mengi kama vile pete za masikio, vikuku, taji, dusumali, mafurungu, vitambi, vibweta vya marashi, matalasimu, pete, azama, mavazi ya sikukuu, vilemba, kitani nzuri, vioo vidogo, debwani, shali, vifuko, utaji, mishipi, nywele zilizosukwa, kisibau.

## VIPODOZI

Kazi ya ngozi, ni kulinda mwili, ufyonzaji au kuondoa uchafu, hisia, kutengeneza vitamini D na kusawazisha joto. Kwa nini watu wanapaka ngozi vitu fulani? Wanapaka ili ngozi 'ivutie,' iwe nzuri, kurekebisha tatizo, kubadilisha mwonekano au kubadilisha umbile la ngozi. Vipodozi hutibu, huzuia magonjwa, na hubadilisha maumbilie. Aina za vipodozi ni krimu, losheni, ointment, poda, dawa za kucha, rangi ya mdomo, kwapani kutoa harufu na rangi za nywele.

Soma historia ya vipodozi katika Wimbo wa Sulemani 1:13-14, Ezekeli 23:40, 2 Wafalme 9:30, Ruth 3:3, Isaya 57: 9, na Mithali 27:9. Neno la Mungu ni mojawapo ya Maandiko ya zamani (ancient literature) yenye ithibati (aunthetic).

Historia ya Wamisri na Wagiriki yaeleza haya yalikuwepo! Vipodozi kama cortico steroids, hydroquinone, mercury compound vina madhara ya kuua cell za mwili, kuleta mzio (allergy), muwasho wa ngozi n.k.

Vipodozi vya kutumika sana ni kama disporone mediven, betnovate, dremovate, betacort au steroids. Hivi huleta chunusi, ngozi kuwa nyembamba na ugonjwa wa moyo. Vipodozi vya quinines na zebaki navyo vina athari mwilini. Vipodozi hivi ni kama body clear gel, mekako cream, rico cream, tura cream, ultra clear soap na butone cream. Hivi vyaweza kuleta muwasho wa ngozi, kansa kuchubuka na mabaka ya ngozi, athari za figo, uziwi, mishipa ya fahamu, ubongo na viungo vya mwili. Vipodozi vya bleach ambavyo watu hujichubua navyo ni kama white cement, bleachers, au jik (chlorite). Hivi navyo vina athari kwa ngozi. Tafadhali peleleza daima vipodozi vipya, vipodozi unavyotumia na kuuliza wataalamu wa afya, watu wa biashara hawajali maslahi ya watu mara zingine, wanaangalia kile kinachokupendeza, na watakuuzia!

Sio vibaya kujirembesha, kunukia au kuvutia au kujipatia ngozi nyororo kama ya Naamani jemedari wa Syria 2Wafalme 5. Ni pale unapoharibu kazi ya ngozi na umbile na kuwa na dhana potofu za uzuri. Mungu ametuumba wote tukiwa wazuri. Pale unapokuwa na dhana potofu kama mtu akiwa mweusi au mweupe ndiyo uzuri, au mengineyo- pua ndogo au miguu mikubwa, maziwa makubwa au kiuno kidogo ndiyo uzuri n.k.; ndipo unapoingia katika shida!

Tujitahidi kuwa wazuri wa ndani ya moyo, baada ya muda watu wataona uzuri wa nje pia. Najua kabisa Maandiko hutaja watu wenye sura nzuri kama vile Sara, Vashti, Raheli, Abigail, Esta, Bathsheba, Shulam, Rebeka, Tamari, Sauli Daudi, Yusufu na Absalomu walikuwa wazuri wa uso. Ila haya mambo yanakuwa mazuri zaidi kama yanatoka ndani na kuonekana nje!

Wasichana wengi wazuri huwa wanaposwa mapema na wengine huolewa hata kabla ya kujenga mahusiano na Mungu na watu. Ni vyema wawe wangalifu ili wasije wakapata mtu asiye mwema ila anayetaka tu mashindano ya kumpata. Wanakuwa vipepeo vya muda mfupi, kisha rangi inapukutika au kufifia kwa kukosa matunzo mema kutoka kwa mume. Tujithamini kama binadamu ambaye aliumbwa kwa mfano wa Mungu. Usafi ni muhimu, na kuwa nadhifu ila mabunifu mengine kuna haja ya kuyatelekeza.

## VIATU

Viatu vivaliwe kutokana na shughuli, usafiri na afya ya mtu. Viatu vya wazi vina uzuri wa kupunguza fungus (kuvu) ila kuna kazi za hatari ambazo miguu inabidi ifunikwe ili isidondokewe na vitu. Wale wenye shida ya fangas au miguu kunuka pengine kuloweka miguu kwenye magadi na siki yaweza kusaidia kiasi fulani. Ulizia tiba rahisi na mbadala, Kausha miguu isiwe na maji maji. Fangasi zingine zinapona kwa kuweka mafuta ya nazi, moringa, majani ya mapema nk.

Viatu vya mchuchumio vilianza kuvaliwa na wanaume wafupi miaka 500 iliyopita, wakitaka kuongeza urefu. Ila wanaume waligundua kwamba vinawakosesha uhuru wakawaachiwa wanawake. Kwa kawaida wabunifu wa mitindo wa viatu, hata sasa ni wanaume. Wangeambiwa wavae viatu ambavyo wanawake wanavaa wasingeweza hata kwa saa moja! Ila wanawake tunatembea na viatu vyenye visigino virefu siku nzima, na hata kama vinawaumiza wanajikaza tu, na wala hakuna anayewalazimisha, ila wabunifu wa viatu hupenda wanawake wavae hivyo! Hivi kwamba kile kisicho na afya, kama wanaume wanakipenda watakivaa tu, ili kuwapendeza, nacho ndicho mara nyingi kipo katika fasheni.

Siku hizi tunaona wengine wanatembea na mfuko wa malapa, wakifika mahali wanabadilisha na kuendelea na shughuli zao na viatu vya kawaida. Viatu vingine vina visigino vya zaidi ya sentimeta 14 kwenye kisigino, na chini ya vidole sentimeta mbili. Nafikiri katika muundo huu, huyu mbunifu anataka mwili wa mwanamke uweze kutoa picha hii: Kwanza, mguu uonekane mfupi na mdogo. Kwa mataifa ya mashariki, kuwa na miguu midogo kwa mwanamke ni urembo. Yasemekana kwamba watoto wa kike China wamekatwa miguu au kuvalishwa viatu vidogo ili mguu usiendelee kukua, la sivyo hataolewa. Madhumuni ya pili ya mbunifu huyu wa viatu virefu, ni kuwezesha, makalio yaweze kutingishika na kutokezea. Tatu ili kifundo cha mguu (ankle) kitingishike ili mtu abaunsi, na kifua kitokezee mbele. Daktari wa miguu Alan Kalker wa Marekani alisema “Kama unachagua viatu vyako kufurahisha macho badala ya miguu, jitayarishe kupokea madhara ya afya.”

Viatu visivyochaguliwa kwa kujali afya vinaleta shida ya kubadili umbile la vidole vikubwa (deformity), huleta vidonda na maambukizi (infection), vinafanya misuli kuathirika na kuwa mifupi na kuonekana kama mhogo au kiazi nyuma ya mguu (contracture of calf muscle). Huleta baridi yabisi kwenye magoti, shida ya mgongo na miguu kupata maumivu, ajali za kuanguka au kuvunjika na kucha za vidole kuingia kwenye nyama.

Utafiti Marekani ulionyesha 90% ya wanawake huvaa viatu vya namba ndogo kuliko wanayopaswa. Pima miguu yako vizuri kabla ya kununua kiatu. *Nunua viatu wakati wa jioni wakati miguu yako inakuwa mikubwa kuliko asubuhi*, na kama unavaa stocking au soksi, basi ziendane na viatu ili zisikuumize. Tumia pesa kununua viatu vizuri na imara, (stable, comfortable) na vyepesi ambavyo vyafanya miguu ipumue vizuri. Usitumie pesa kununua viatu vingi visivyo na afya! Uwe na viatu vichache imara, na vyenye afya! Hata nguo ni hivyo hivyo,

nunua nguo chache zenye afya, zinazotengenezwa kwa malighafi ya asili kama, hasa zile zinazogusa mwili, hivyo unaweza kuweka lining.

Tunza miguu isipasuke pasuke; paka mafuta, miguu iliyopasuka inaingiza bakteria na yaweza kuchana matandiko. Kula vyakula vya asili vya mboga-mboga na matunda hupunguza mipasuko Vaa viatu, na safisha vizuri miguu, maana udongo mwingine ni rahisi kupasua miguu. Usisimame muda mrefu, na punguza uzito kuisaidia miguu yako. Ni bora kutembea muda mrefu kuliko kusimama muda mrefu kwa miguu! Tunza miguu yako vizuri inalinda afya yako na kama una kisukari, angalia kama una mkwaruzo hata mdogo maana vidonda haviponi haraka. Wengi hatujali miguu sana kama uso, ila miguu na kucha zake ni kielelezo (indicator) cha afya. Kama una shida ya miguu kupasuka-pasuka, shida ambayo mimi nimekuwa nayo zaidi ya miaka 25. Mrs Msusu wa Morogoro, alinipa ufumbuzi rahisi sana “Chukua mafuta ya Vaseline na dawa ya mswaki kama Colgate, changanya pamoja, osha miguu asubuhi na jioni na paka, baada ya wiki tu utaona mabadiliko makubwa,waweza kuongeza kiungo kinachoitwa minjano-tumeric”. Hii haina maana dawa ya mswaki ya Colgate ni nzuri kwa afya yako! La! Jifunze vitu vya asili vya kusaidia meno, ikiwemo-chumvi na mafuta ya nazi uchanganye pamoja kwa uwiano wa 1:3 na upigie mswaki, unga wa mkaa, na miswaki ile ya miti, ni msaada mkubwa.

Jambo la ziada ni kwa wale ambao miguu hupasukapasuka, hii ni rahisi kutibu, chukua mafuta ya vaseline na dawa ya mswaki kama vile colgate nk, weka kwenye miguu iliyopasuka uendapo kulala mpaka asubuhi, kwa kawaida ni wiki moja mpaka nne tu, inayotakiwa kwa miguu kurejea katika hali yake nzuri!




## NGUO

Nguo ina uhusiano mkubwa na afya, iwe kujilinda na hali ya hewa, mazingira, sare, kazi au uchafu. Nguo zimekuwa tatizo la miaka mingi toka pale Adam alipojitengenezea vazi lake mwenyewe kutoka kwenye majani ya mkuyu. Alijifunika kwa udogo, nguo ambazo hazikufaa wala kumstiri mke wake mpaka Mungu alipowatengenezea nguo kutoka kwenye ngozi ya kondoo. Lengo la Mavazi la kwanza ni kuficha uchi, ili tusipate aibu, kwanini tufiche utupu? Kwa sababu Muumba wetu amesema, kituo kikubwa (.).

Kila mtu ana utupu au uchi, na utupo sio wa kuonyesha kwa watu tupitapo barabarani. Kila mtu anao utupu. Ni aibu kwetu kuonyesha uchi kisaikologia na sababu nyingine. Lazima tujiulize

tunapovaa, je, mavazi yetu yanatusaidia afya? Je, yanatusitiri, yanatusaidia kijamii, kiroho, kiuchumi au kimawazo? Je, tunavaa kwa utukufu wa Mungu, au kujionyesha watu watuone. Waweza kufikiri ni jambo dogo ila mambo ya mitindo yameumiza wengi. “Tazama Naja kama mwivi, heri yule akeshaye na kuyatunza mavazi yake, asiende uchi hata watu wakaiona aibu yake,” Ufunuo 16:15. Haruni aliambiwa avae mavazi ya “mavazi matakatifu, kwa utukufu na kwa uzuri.” katika Kutoka 28, ikimaanisha wazi kwamba kuna mavazi yasiyo na utakatifu, utukufu au uzuri, hivyo unapovaa jiulize haya maswali matatu kuhusu mavazi, ndiyo kiwango au kipimo na kanuni. Soma Sura ya 28.

Hata wanaume wanapaswa kuvaa mavazi ya heshima, wasiache suruali zinazodondoka. “Kisha utafanya kanzu kwa ajili ya wana wa Haruni……. nawe wafanyie suruali za nguo ya kitani, ili kufunika utupu ya miili yao; suruali hizo zitafika tangu kiunoni hata mapajani……… nao watazivaa watakapoingia hema ya kukutania … wasije wakachukua uovu, wakafa; hii itakuwa amri ya milele kwake yeye na wazao wake.” Ndugu zetu Waislamu wanavaa kwa heshima sana hebu wengine, wawe waangalifu ‘kuwakwaza watu na kuishi dini ya kukosa kicho.’

Nchi za magharibi wana sehemu za jumuiya za kuogelea bila nguo, au wanaenda kwenye hoteli maalum. Kwingine wanaenda na watoto wao wakiwa uchi bila nguo (nude Beach). Mambo haya yameongeza uchafu wa uasherati, na mtu kujamiiana na watoto wake (incest), ushoga na machafu mengine mengi tu. Kutafuta uovu, Sio kuwa mtu wa maendeleo, hata watu wasiomjali Mungu wanawashwa masikio wakisikia uouvu na vituko hivi. Mungu alituambie tufiche utupu wetu kwa vile nuru Yake haikutufunika tena na dhambi yetu.

Nilitembelea nchi fulani za ulaya, na kukuta watu hawavai nguo wakiwa ndani ya nyumba zao na ukipiga hodi wakikuona kwamba wewe si wa pale wanakimbia kuvaa nguo zao! Nikiwa na rafiki yangu Iyaya tulimwona mama mmoja anafagia mbele ya nyumba yake bila nguo hata moja, ila alikuwa na viatu! Tukamwona bwana mwingine anatengeneza bustani bila nguo. Alipotuona alipiga mbio, na rafiki yangu akamwambia, “Baba kama ulitaka watu wakuone, unakimbia nini?”. Aliend kuvaa akatoka nje tena. Hawa wote walikuwa watu wazima wa miaka 40. Na cha kukazia, ni kwamba hata kama walitembea bila nguo, walijua kwamba ni kosa, ndiyo maana walipotuona, walikimbia na kwenda kutafuta nguo.

Je, umeona ndugu msomaji, kwamba hakuna asiyejua kwamba kukaa uchi siyo vizuri? Wangekuwa hawajui wasingekimbia. Hata rafiki yangu mwingine anayefanya hospitalini aliniambia, “Hivi hawa watu wanaonyesha nini? Mbona kila mtu anacho hicho hicho walicho nacho?” Nafikiri wewe hutapenda kujitembeza uchi au nusu uchi bila sababu. Ukiwa mwanamke utajiingiza kwenye matatizo ya kubakwa, kutokubaliwa na watu au kutokubaliwa kuhudumu. Ni vizuri nguo za wanawake ziwe tofauti na wanaume. Wataalamu wa maandiko ya zamani wanasema kwamba wote walivaa kanzu za heshima na kaptura ndani, ila rangi zilitofautiana.

Watu wengi wanasema wavae tu kama jinsia yoyote kwani wanawake na wanaume ni sawa isipokuwa viungo vya uzazi! Hii kauli imetoka nje ya mstari. Ni kweli wanawake na wanaume ni sawa mbele za Mungu ila kuna tofauti ya maumbile na shughuli au utendaji (function) kutokana na uumbaji. Sasa wewe kama unataka kuleta hili kwenye jumuiya yako utaiharibu, umeshaona

jinsi tunavyopamba na ushoga kama waaamini na serikali. Mwanamume anaweza kuvaa kaptura tu, na kuendelea kulima shamba, ila wewe mwanamke unaweza kweli? Mwanamume ana sehemu au maumbilie yake na mwanamke pia. Mavazi yaonekana kuwa kitu kikubwa cha binadamu na hata katika ibada ya Kweli.

Tunaona wanawake wawili wamewekwa kama mifano ya ibada ya Kweli ya Mungu na ya adui au Yezebeli. Ufunuo 12 na 17 yaelezea kidogo. Sio heshima nzuri kuvaa nguo zenye maandishi ya kukashifu watu 'mtajijua wenyewe nk', kutumia visivyofaa au kukaribisha ugeni usiofaa. Watu wamevaa Tshirt za "Tumia pombe ya chibuku." Niliona msichana amevaa tshirt iliyokuwa imeandikwa, "I am available!" yaani yuko tayari, sikuwa na uhakika kama ana utayari kwa mema au mabaya. Sentesi za kuelea hewani hazina maana au heshima kwa mtu. Nyingine "Njoo unichukue, mimi ni wako," au "Natafuta mwanamke tajiri nimwoe;" n.k. Najua twanunua mitumba au kuvaa kanga mara zingine bila kusoma. Je, wewe unatafsirije maneno haya ukimwona nayo mtu? Watu wanakusoma akili yako kirahisi kwa mavazi yako na kukuweka kundi fulani. Na ukizungumza wanakuwa hawatilii Makini, sembuse utakapowaletea habari njema? Siku ukihitaji kazi katika mahojiano wanaona wewe ni mtu usiye na maadili yaani ni muhuni wa mtaani tu. Wanakuwa wamekusoma kwenye facebook, instantgram, whatsapp,

Nguo zisizo na afya ya kimwili na kiroho ni zile ambazo zinakuwa fupi, zinamtukuza mwanadamu badala ya Mungu, zinaonyesha sehemu za mwili kama kifua, mapaja, zina mikato mikubwa au zimebana mno au zinaleta baridi au joto au usumbufu badala ya faraja. Nguo hizi nyingine ni nzito upande mmoja, zinafagia barabara na kuchota takataka, au zinaacha miguu isikie baridi. Naelewa mara zingine kwa kweli inatokea bahati mbaya, nguo hujaiona muda mrefu au mpya na unavaa kwa haraka,ili uende mahali kwa dharura  na kugundua ina hitilafu. Ila kama ni kitu cha kupanga ni vigumu. Mama zetu ndiyo maana daima walitembea na kanga na pini au hata sindano kwenye pochi zao, alimradi wasijiabishe!

Kuna magonjwa mengi yaletwayo na mitindo ya nguo zisizoendana na afya. Watu wengi wanauawa kwa fasheni kuliko tunavyofikiri. Mfano wa magonjwa ni kama vile: mapafu kubanwa, mishipa ya fahamu na ya damu kubanwa, vichwa kuuma (damu pungufu ubongoni), myeyusho wa chakula kuathiriwa, damu kutoka puani n.k.

Kwa wale waumini wanaotaka kuwa na afya ya kiroho "Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni." Kila mtu ana jukumu ya kutunza afya yake ya kiroho ila unapovaa nguo na kuwakwaza wengine kuna walakini. Wanaume wanavutiwa kwa kutazama jinsia nyingine na wanawake wanavutiwa na mwanamume anayejali au kuwaonyesha upendo. Usivae nguo bila kujali watu, na hata kama ni wanawake wenzako kwa nini ujiabishe na una utume mkubwa hivyo? Maana una baba, Wana wa kiume, kaka, binamu, na wajomba, utapenda ndugu zako hawa wa kiume wakwazwe kweli au kujipatia sifa mbaya?

Wafikiri watu wanaompenda Mungu au watu waliotilia makini vitu vyema wangevaa hivi ? Je! Kama Leo ndiyo ingekuwa nakutana na Mwenyezi Mungu, uso kwa uso, ningevaa hivi kweli?

Kama jibu ni la, nenda ukavue na kuvaa nguo za adabu. Hiyo pia inahusu vile vitabu tunavyosoma, zile picha tunaangalia, au hata ule umbeya tunaoeneza.

Nguo inakuletea sifa mbaya au nzuri. Nguo nyingine zapaswa uvae ukienda kulala na sio kutembea nazo barabarani. Mara nyingi tumejisahau katika kuwavisha watoto wadogo wa kike nguo kama vikaptura vidogo, nguo zisizo na mikono, mikono ya mikanda inayoacha kifua na mgongo wazi n.k. Wakiwa wadogo sana haina shida ila ni vigumu kujua ni wakati gani wa kuacha kwani sio watoto wachanga tena, na huenda watakuwa wamekwishazoea! Watoto wengi wadogo waliozoea kuvaa sururali za kubana na kukosa adabu wakiwa na miaka mitatu, inakuwa vigumu kuwaambia sasa mmekua wakubwa, toeni hizi nguo kwani zaonyesha sehemu nyeti.

Watoto waliozoea kuvaa suruali, imekuwa vigumu kukaa vizuri wakivaa magauni, na hapa ni vyema labda kuvaa kama Agano la Kale, kwamba chini ya gauni mtoto avishwe kaptura n.k. ili hata wakikaa kwenye jukwaa, iwe sawa. Wanawake wengine tumepatikana na shida ya namna hii, kwani suruali zetu nyingine zinabana mno na mara nyingi hatuna mashati marefu au koti la suti la kufunika sehemu hizo, na kila mtu anaona herufi ya V kwenye sehemu yetu ya siri.

Wote wanaopenda kujistahi tusaidiane kwa haya na yale ya kupasua nguo (slit). Mara nyingine tunavaa nguo mpya kwa haraka na hatuna mtu wa kutuambia kwamba kuna hitilafu, na kujikuta tuko mbele ya watu na hata watoto na nguo isiyo ya heshima. Nchini mwetu si shida, ila napoishi nimeona mara kadhaa wanawake walioenda na nguo fupi mimbarani, na kuonyesha mapaja au hata chupi wakiwa wamekaa kwenye viti wakitazama watu. Wengine walijaribu kuzivuta nguo ziwe refu, kana kwamba hawakujua urefu wake. Au wanafunika na Kitabu Kitakatifu. Tumeshukuru kwamba mambo hayatokei kama vile yalivyotokea wakati wa Torati! Maana mtu angesimuliwa kwamba ameanguka Pu! Mbele ya watu.

Mitindo yaweza kupunguza unyenyekevu. Tumeona watu kwenye nyumba za ibada, hasa makanisani, maana misikitini wanawake wanavaa kwa heshima sana. Wakati wa kuingia kanisani na vinguo vya ajabu kuabudu, twataka watu watuone kwamba tuna vitu tofauti na wengine. Viatu vya michuchumio vyawekwa hata misumari chini ili vilie, kujitembeza hapa na pale bila sababu. Kutoka nje na kurudi tena ibadani ili tuwe maonyesho.

Kama una majaribu la kujionyesha, anza kuchagua mavazi machache tu ya adabu utumie. Ukiona kwamba majaribu yako ni kujionyesha, jaribu kuchagua vitu vichache tu ili usikoke moto zaidi kwa dhambi yako ikuzingayo kwa wepesi. Msemo wa Mungu wa ‘afadhali uwe chongo na kwenda mbinguni;’ ni kweli kabisa. Hatuko duniana kwa mashindano, au maonyesho, wala maonyesho ya mitindo, au umimi wa kujifikiria. Tusipoteze malengo ya watu au kuwakwaza baba zetu, kaka zetu, waume zetu au wana wetu.

Maswali ya kujiuliza kuhusu mavazi ni Je, NAPOVAA nguo nasema Moyoni, wacha nivae leo kwa Utukufu wa MUNGU? Je, napoweka rangi kwenye makucha, napochana nywele zangu au kusuka au kuweka chale

au kupaka rangi mdomoni, au kuvaa tai au pambo lolote, naona kwamba nafanya vile kwa utukufu wa Mungu?

Kuharibika kwa afya kwaajili ya fasheni, hakumletei Mungu Utukufu. Kuvaa ni fasheni na pia utamaduni, mfano mwanamke wa Kihindi anapovaa sari, huwa anacha tumbo nje! Je,

sisi tuvae kwa utamaduni wetu au kwa fasheni au kwa kumtukuza Mungu? Hakika tumtukuza Mungu iwe kipaumbele, na kisha utamaduni na fasheni namba mbili. Kwani fasheni na tamaduni nyingi zina mavazi mazuri tu, ambayo unaweza kuyafanya yaweze kumtukuza Mungu bila ya kukugharimu chochote zaidi. Je, nguo zangu zikoje? Je, ninavika yatima, wajane na masikini, kabla ya kujirundikia nguo nisizozihitaji, au

ambazo sio za lazima?

## NYWELE

Zamani hatukuwa na shida sana ya nywele ila siku hizi watu wa nchi zingine wametuletea fasheni nyingi za nywele, wigi, vipini, plastiki nk. Na wengine wetu tumejisikia hatuna nywele nzuri, au lazima tukazane sana kwa mambo yahusuyo nywele, mpaka zawadi ya Mungu a nywele ikawa mzigo. Nimesikia dada wengine wakisema "leo sitatoka nje kwani sijapata msusi wa nywele zangu." Nywele zako ni sehemu ya mwili, kama pua na mguu, zisikufanye uwe mtumwa, jifunze jinsi ya kuziweka vizuri mwenyewe kwanza, ndiyo mtu mwingine akusaidie. Usafi na unadhifu ni muhimu, ila kujionyesha ni jaribu letu binadamu wote. Wengi wanafikiri kwamba ni lazima msichana akate nywele ziwe fupi sana au upara. Kwa kweli sio dhambi msichana kuwa na nywele ndefu. Inatofautisha tuonekane na sura ya kike kwa wengi wetu. Wengi tulifikiri kwamba ni rahisi kuvaa kitambaa au kuvaa wigi ili kumudu nywele au kuokoa muda. Kuvaa kitambaa, kofia au wigi kunaleta upara kwa usugu na kufanya nywele zisipate hewa. Sio jambo la afya kufanya hata hivyo tuliumbwa na nywele kwa ajili gani? Nashauri kama unaweza kufunika nywele kanisani, litakuwa jambo zuri, angalau tunajua imeandikwa, kama siyo jambo zito, basi angalau tumetii tulivyoelewa, naona Mennonite wa Marekani wakifanya hivi, na wanaonekana vizuri kabisa!

Madawa ya nywele ni mengi siku hizi, kwanza saluni nyingi hazina hewa ya kutosha na kuna mivuke ya hewa mbaya zenye kemikali za dawa za nywele (volatile organic compounds and carcinogenic). Utafiti wa Marekani ulionyesha kwamba watengenezaji wa nywele wana riski/hatari kubwa ya kansa ya damu (Leukemia) na zingine kwa vile kila siku wanakuwa katika mazingira ya kemikali kama ammonia, hydrogen peroxide, fomaldehyde na Phenylenediamine na zinginenzo. Waweza kupata maelezo zaidi kuhusu yote haya. Rangi za nywele (kanta) ambazo zimefanyiwa upelelezi na kukutwa na mengi yanayodhuru afya wengi wetu tuliona utafiti huu wakati mke wa JF Kennedy alipokufa Jaqueline Onasis na lymphoma. Jaribu kufanya vitu vyako viwe vya asili, kwa kufanya nywele nyeusi tumia unga wa mkaa na hina pamoja! (Hina na rangi ya asili ya Indigo nk) Hata hivyo ni heshima  pia kuwa na kitu cheupe, ila wanawake wengi wanapenda kuonekana vijana, na wanaume wengi siku hizi wameingia hapo pia! Kila kitu kifanyike kwa kiasi, ukiomba hekima kwani hakuna aliyewezea, hata tunapoandika tunashindana na haya katika maisha yetu kila kukicha. Kuna pambano kuu, kati ya Mungu na

tabia yake na Shetani na chachu yake. Bwana tupe nguvu.

Tunaona Yezebeil bibi mwovu “Akapata habari, akatia wanja wake machoni mwake, akapamba kichwa chake akichungulia dirishani.” Huyu mama tunamtaja kwa sababu, japo “Alijishughulisha kupamba mwili, hakushughulisha kupamba roho.” Haya ni mambo ambayo yana utata sana, ila mtu anapoendelea na safari ya kumcha Mungu na kuishi maisha ya kiasi na utauwa anagundua vya kuacha na vya kuendelea navyo. Kila mtu yuko kwenye ukurasa tofauti. Mbunge Charles Schumer wa Democratic NY alisema kwamba wanatafiti lipstick, rangi za macho/uso, na hata nguo za shamra (costume toka uchina) na viwango vyake. Hii ni kwa sababu shirika la viwango limeona kwamba nyingi zina chuma cha Lead, Nickel, Cobalt na Chromium. Chuma cha Lead ni kitu ambacho hakina usalama kwani kinaathiri ufahamu wa mtu. Wengi huwadharau na hata kuwacheka watu wenye ‘tatoo’ ila wanapaka rangi za kucha, nyusi na midomo, hii ni sawa tu na tatoo. Sisemi kwamba vitu hivi ni vibaya, la! Mungu anajua, ila vyote ni kitu kimoja tu! Au wewe unafikirije rafiki? Tofauti yake ni nini?

Biblia inasema, “Kujipamba kwenu kusiwe kujipamba kwa nje, yaani kwa kusuka nywele na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi, bali uwe utu wa moyoni usioonekana katika mapambo yasiyoharibika; yaani roho ya upole na utulivu, iliyo na thamani kuu mbele za Mungu.” Fungu hili la Petro wa kwanza sura ya tatu liliandikwa baada ya kuonekana kwamba tunajaribiwa mara nyingi na kujionyesha kwa vitu vya nje. Kuna kujipamba ambako kunapita kiasi. Naelewa kusuka kwa nywele za wazungu ni tofauti, na zetu ila anachomaanisha, ni jambo la kufanya tukipita mpaka, na kuwa na nia ya nje ya vile Mungu anataka tuwe nayo.

Mhubiri mmoja kutoka visiwa vya Barbados, aitwaye Randy Skeete akiwa Nairobi kanisa la Maxwell, aliwaambia kina dada, “Hivi Bwana Atakapokuja kutoa thawabu siku ya mwisho atawawekea wapi taji? Mmeshajipamba kichwa kila mahali wala hakuna nafasi! Mna- shanga, vipini, vitambaa na kadhalika!” Wengine wanasema kwa vile tumeandika taifa letu kwenye bangili zetu. Nafikiri hii ilikuwa ni futuhi, ila ilinifanya nifikiri-Angalia mahubiri yake kwenye tovuti; ni kweli tunapoteza muda mwingi kwenye kujipamba badala ya kujali maisha yetu ya kiroho. Je, masaa yale tunayoshughulikia vioo, na nywele ndiyo tunayoshughulika kuhudumia jamii zetu ili ziwe bora na tabia njema na kusaidia wenye mahitaji kama wajane, yatima na masikini. Je, tunatumia muda kujenga mahusiano na Mungu kwa kusoma Neno Lake, ibadani na sala?

Wigi nyingi zimetengenezwa na mikia ya farasi, plastiki, na nywele za watu wengine. Na hizi zinaleta joto miilini mwetu na uzito kichwani mwetu. Pia zinafanya usafi wa nywele kupungua; maana ukianza kuvaa wigi, inakuwa vigumu kuchana nywele zako tena na upara upo njiani mapema. Unashikwa na uvivu, na kipara kinaanza kirahisi, maana si mpango wa asilia kuwa na wigi! Wengi wetu tunafikiri tuna nywele mbaya ila wazungu au wahindi ndio wana nzuri! Aliyekuumba hajakwambia ni mbaya, usidanganyike. Na tunapozoea vitu vyao, vyetu hatuvipendi. Zamani watu walipenda vitu vya asili, leo magharibi inatuelekeza kwenye vitu ambavyo si vya kutusaidia sana, nao wamegundua na kuviacha, sisi tunabweteka kwanini?

Rafiki yangu Boni wa Zimbabwe siku moja tukifanya naye kazi alinipa kisa cha ajabu. Kwamba; "Niliona matiti yangu ni makubwa, hivyo nikaamua niende kupasuliwa yapunguzwe! Nikamwambia mume wangu, naye akashangaa akasema, mbona mimi sijalalamika?" "Ukimaliza huo upasuaji, badilisha anuani yako!" Alisema mumewe aliona pengine alitaka kufanya hayo kuwafurahisha wanaume fulani, na hivyo ahamie kwao. Dada huyu alinipa moyo sana, maana kila mtu ana kitu fulani hakipendi mwilini mwake, na pengine hata watu wanamwongopea hivyo. Watoto wangu huniambia mara nyingi mama una pua kubwa etc. Sasa ikiwa kubwa nifanye nini? Mungu aliponiumba Yeye katika hekima Yake aliona inanifaa. Yabidi niangue kicheko tu na kuendelea mbele, nikikutana na wenye pua kubwa na vitu vingine vyenye kasoro kama mimi, tutajiunga sapoti grupu. Hata hivyo na uzee sasa nimekuta maumbile hata yaliyokuwa ya kawaida sasa hayapendezi. Nangoja Mungu kunipa uzuri Wake siku moja aliandika mama mmoja kwenye tanzia yake Kule Lake George New York nilipoenda kwenye makambi mazuri ya familia (Restorationinternational.org)

"Dear God I have tried (but failed) to do my best

Now here in dust will rest

Until in glory You return to give me life

I have not earned, with my last breath (in hope)

I pray. Remember me on that great day

When You come to ressurect people

To come out from their graves

To live with you forever in heaven

In your precios name I pray"!"

**Tafsiri**

Mpendwa Mungu, nimejaribu wee (ila nimefeli) kufanya niwe mzuri kwa uwezo wangu

Na sasa nimelala mavumbini (kaburini) nikipumzika

Mpaka katika siku ile ya utukufu utakaporudi kunipa uzima wa Milele

Nakuomba Mungu wangu unikumbuke siku ile kuu

Utakapokuja kufufua watu watoke makaburini walipopumzika wakikungoja

Ili waishi Nawe Milele zote mbinguni BABA

Si kwa uwezo au nguvu zangu BABA, bali ni kwa upendo na rehema Yako tu

Ni kwa Jina Lako Kuu ninakusihi leo.

Ubaya ni kwamba tunapoanza mambo haya yanaonekana madogo, ila watoto wetu wanayaiga

na kuyaongezea chumvi, mpaka tunaonekana kama tuko kwenye mchezo fulani wa kuigiza (drama).

Vyanuo au kofia za moto zina madhara kwenye kichwa, na hasa wakiweka kemikali kwenye utosi. Watu wengi wamepoteza nywele. Spray za nywele na hata poda nyingi zinaathiri mapafu. Mambo ya kujipamba nywele yamekuwepo kwa maelfu ya miaka. Kwa kweli nywele ni utukufu wa mwanamke na humrembesha; mwanamke usijiachie ukatisha, ila uwe na kiasi. Tushughulikie yale ya muhimu kwanza. Nywele zisafishwe mara kwa mara. Watu wengi wanakaa mwezi mzima bila kuosha nywele, huku zimefunikwa na wigi; ila wanaoga mwili. Hiki ni kitu cha kuleta madhara. Mwili na nywele zinachafuka kwa njia hiyo hiyo na kupata jasho na mafuta hayaoshi vizuri nywele kama maji. Maji ndiyo solution bora kupita yote kusafisha mwili. Injini ya gari ndiyo yasafishwa na mafuta si mwili wa binadamu.

Tumia chanuo lako mwenyewe na kama yabidi uazime, hakikisha limeoshwa na sabuni kujilinda na magonjwa ya ngozi au chawa. Nywele zisizotakiwa mwilini kama vile kwenye videvu vya wanawake, tumboni au pengine zikatwe na mkasi na sio kukwaruzwa na wembe. Nywele zahitaji protein ya Keratin hivyo lishe ni muhimu. Tengeneza shampoo nyumbani kwa asali, aloe vera, shea butter na mafuta ya nazi. Upungufu wa madini kama zink au vichocheo vya mwili vyaweza kuathiri nywele. Nywele mara nyingi zaweza kueleza afya zako zikipungua upana (thickness), zikiweka njia panda kwa kupasuka, au zikibadilika rangi. Kila nikiangalia nywele zangu nagundua hili.

Nywele ni pamoja na vinyweleo, nyusi, kope na zile za sehemu za siri. Vinyweleo husaidia ngozi kutoa takataka za mwili na kusaidia mwili usiathiriwe na vumbi au jasho. Nywele za kwenye sehemu ya siri, (mavuzi) zinasaidia usafi, kupunguza unyevunyevu, muwasho, kunuka n.k.; pia hupunguza baktiria. Inashauriwa mtu asinyoe nywele hizi zote abaki upara. Michubuko ya makali ya wembe au kemikali za kuondoa nywele inatoa mwanya kwa bacteria au virusi kupenya. Ngozi iliyoachwa wazi bila nywele hupata athari inapogusana na jasho lenye taka toka mwilini. Punguza kwa mkasi nywele hizi, ziwe fupi kadiri inavyowezekana. Uoshe nywele za mwili, kila siku na kuzikausha ili usilete unyevunyevu na kisha fangas au baktiria. Nimesikia watu wengi wakisema hawahitaji deodorant ya kukata harufu mbaya ya jasho. Nikasema ni kweli kabisa, ila watu wengine walio karibu yako ndiyo watakwambia kwamba huhitaji, maana wengine jasho lao halinuki au watahitaji uweke kitu ukiwa karibu nao. Watu wachache sana ambao hawana harufu ya kwapa, ila wengi tuliozaliwa karibu na ikweta tuna tezi za jasho nyingi kuliko wale wa nchi za baridi. Watoto wangu wadogo wa miaka 10 tu nimesikia jasho likinuka na hii si nzuri wakiwa na wenzao, maana watoto hupenda kukashifiana. Chagua njia rahisi za asili kama chumvi (Thai salt bar). Hii ni kama dola 6 hivi ila waweza kutumia hata kwa miaka. Hata waweza kutengeneza yako. Waweza kutengeneza mwenyewe deodorant ya kwapa, lisiwe yenye harufu kali! Vijiko vya 4 mafuta ya nazi, 2 baking soda, 2 corn starch au cassava starch na ongeza harufu ya mafuta ya mkalatusi, au mint ukitaka nk! Hata dawa ya mswaki pia tumia hivi vitu au mkaa au miswaki ya miti kama vile muarobaini nk. Vijiko 4 vya mafuta ya nazi, vijiko 2

baking soda, vijiko 2 chumvi ya mawe au himalayan, na udongo wa mfinyanzi wa bentonite, huu unaongeza kusafisha meno zaidi.

Kope na nyusi huondoa vumbi na uchafu unaotokana na kuganda kwa mafuta na vipodozi tunavyopakaa. Kukata nyusi si jambo jema ila zipangilie vizuri. Hata kwa wale wenye nyusi nyingi ukinyoa zinaota nyingi zaidi; ila ukiziacha zinaendelea vizuri. Hili nalo ni chaguo la mtu, ila ukianza zinazidi kuwa nyingi. Zamani watu hawakukata nyusi na kila kitu kilikuwa sawa! Labda uwe na shida maalumu kubwa ya kuwa na nyusi nyingi kupita kiasi, wewe ziache. Sidhani kama uzuri unatokana na nyusi na kope sana japo wengi wanabandika kope bandia siku hizi, Krimu za kuondoa nyusi nyingi ni mbaya kwa vile zina kemikali na kuleta mwasho au shida za macho. Mara nyingi unapofanya vitu vingi, unaongeza shughuli nyingi, na unapokuwa na haraka au ukizeeka, unaanza kuona pengine unaonekana kituko. Ila yote tunayoelezea ni maoni tu, wala si amri. Ila usichekeshe watu sana!

Mvi mara nyingi huja baada ya miaka 40; ila urithi, vichocheo, kemikali, vileo, sigara, na vyakula vyenye acid nyingi vyaweza kuleta mvi mapema.

Wanawake wengi wakiwa watu wazima (menopause) na kuacha hedhi, wanaanza kuota ndevu. Hii ina changamoto ya kisaikologia. Akiwa msichana mdogo hali ni ngumu zaidi. Pengine ni vizuri apimwe homoni/vichocheo na kushauriwa. Mwanamke anapenda aonekane kama mwanamke bila ndevu, hivyo kama unataka kutoa mashauri ukate kwa mkasi badala ya kunyoa. Maana zitakuja nyingi zaidi. Itabidi wasichana wadogo watafute ushauri zaidi wa matabibu kuhusu vichocheo hivi. Ila usitumie vitu vikali, vinavyodhuru mwili.

Baadhi ya sababu zinazofanya ndevu kuota ni:

Vichocheo kuzalishwa kwa wingi kwenye mfuko wa uzazi, uvimbe kwenye mfuko wa mayai, matumizi ya dawa za majira, matumizi ya vipodozi vyenye dawa za vichocheo vya wanaume (testosterone au steroid), uvimbe wa tezi la karibu na figo (adrenal), unene wa kupindukia-unaleta vichocheo vya wanaume (androgen), na mabadiliko mengine mwilini. Ulimwengu wa leo wa vichecheo umeleta shida kwa wanawake na wanaume ambazo hazikuwepo. Peleleza habari hizi zaidi kwa wanasayansi.

Kwa wanaume, ukifuga ndevu zitunze ziwe safi na ziwe zenye mkato mzuri. Ukiamua kunyoa ndevu hakikisha unanyoa kwa unadhifu. Nywele zako pia ni vizuri zisiwe ndefu sana. Mambo ya kusuka rasta ni magumu kuyaratibu, hatushauri ujiingize kwenye rasta, uwe mwanamke au mwanamume. Shukuru ulichopewa na Mungu, acha kichwa kipumue.

Kufuga nywele kwa wanaume kunaleta mwonekano wa kukataliwa mahali pengi Afrika. Labda kwa wanamuziki au vijana wanaojifanyia shughuli zao wenyewe, hivi kwamba hawatajali wakikataliwa. Ila kama mtu anafanya kazi kwenye umma kama Tabibu, cashier, mwalimu inakuwa shida hata kuipata kazi, na akiipata mara nyingi mwajiri wake angependa azikate, ili kutunza picha ya anapofanyia kazi (image). Je, wewe ungekuwa unaajiri mtu kwenye kampuni yako ungemwajiri mtu anayefuga nywele ndefu na hachani? Kuna kijana tulikuja naye nyumbani

na alipaswa kuzungumza na watu wengi katika mkutano, watu walimsihi akate nywele maana si heshima kwa utamaduni wetu. Kijana huyu alibishana basi ikabidi atolewe kwenye ratiba.

Walimwambia kwamba kwa vile ameshafika Afrika, atapelekwa kutembezwa kwenye mbuga za wanyama (Serengeti Safari park) bali hawezi kutoa hotuba za heshima. Nafikiri dhumuni lake halikuwa kuja kwenye mbuga za wanyama, hiyo ilikuwa ni bonasi, hivyo alikata nywele mara. Kubishana na watu kwa mambo madogo, madogo, inafanya tusikue. Mambo mengine yachekeche Wafilipi 4:8, na kama hayakugharimu sana yafanye. Wanaume wengi wa visiwa vya Jamaica toka udogo waliacha nywele ndefu, kwani mama zao waliamini wasikatwe nywele mpaka waweze kusema, ikiwa kama imani ya namna fulani na baada ya hapo waliziachia tu na kuzivingirisha na kuvaa kitambaa fulani (rasta). Wengine walikuwa wamekaa nazo kwa miaka 30 na zilikuwa kama futi tatu au nne hivi. Mahali pengine waliuza nywele zao kwa mashirika fulani. Pengine ni mradi mzuri!

Rangi na kucha bandia zinaleta maambukizo ya kucha na kupoteza kucha, kupungukiwa na kucha vidoleni, au kuwa na vipele karibu na ngozi ya kucha. Kucha bandia zinafanya ukucha usipumue na kufanya kazi zako inakuwa shida sana, ila angalia pia watoto na watu karibu watakuigiza, na utakuwa umepanda mambo ambayo siyo ya lazima!

### Rangi za midomo

Jiulize, je, nahitaji mapambo haya yote? Rangi hii si nzuri kwa afya, hasa ukitumia kila siku; na zaondoa rangi ya asili kwenye ngozi (pigmentation) na yabidi upate za asili maana zingine zina madini ya lead (risasi). Kama inabidi kutumia tengeneza mwenyewe zako, na ujiulize, Je, nafanya hivi kwa utukufu wa Mungu, maana muda wa kufua nguo, kuoga, kupaka mafuta, kupasi nguo, kuchana au kusuka nywele ni mwingi tayari, sasa kwanini ujiongezee kazi. Na unapokula na kunywa kitu ule kwa staili fulani ili isitoke, au utoke hapo ukaiweke tena. Inakuwa kazi ya siku nzima. Na lengo lake ni nini? Nani unayetaka akuone sana? Bwana au bwana?

### Rangi za macho:

Hizi zaweza kuleta maambukizo ya macho, ngozi, upofu, vinyweleo, muwasho, kansa ya ngozi, allergy-mzio, vipele, kope kuanguka, n.k.

### Krimu, losheni na shampoo:

Zaleta macho kuwasha, ngozi kudhurika, muunguzo wa ngozi, rangi kubadilika, vidonda, damu kutoka, ngozi kuwa pana, kansa ya ngozi, kubugudhiwa na jua (sun sensitivity). Mara nyingi watengenezaji waandika ni vitu vya asili (natural). Asili haina maana kwamba ni 100% pure, salama na safi. Kuna mimea mingi ina sumu ya kuua, inadhuru au inalevya! Hata kama ina vitu vya asili ina kemikali! Baktiria, mbolea za viwandani, au dawa za kuua wadudu zimetokana na vitu vya asili.

Watu wakitumia rangi za macho au mascara ya macho wanalowesha brashi ya kope na mate na kuleta maambukizo, wanalala na rangi na kuathiri macho, wakiwa kwenye joto la zaidi ya

32C; wanafikisha macho na hizo rangi zaingia kwenye macho na kuathiri kioo cha jicho (cornea), wanafanya kope zidondoke, au shida ya kutoona vizuri na upofu.

Mara zingine vito na urembo vinahusishwa na uasi, uasherati, uzinzi, au kutongoza wanaume. Hivyo tungependa kusema vifanye kwa kiasi. Tuwe na kiasi maana kila mtu akiwa na utajiri wake na akauonyesha kwa kujiwekea dhahabu hapa na pale yatakuwa maonyesho haswa. Kama una mali, zitumie kwa  kusaidia wenye mahitaji. Basi usizitundike-tundike wakati ni rasilimali kubwa ya utume.

Siku hizi hata wanaume wanajipamba, kwa kuvaa vipuli n.k. Zamani hata marashi ya kujipaka hayakutumiwa na wanaume. Siku hizi wanaume wana marashi makali, pengine kupita wanawake! Vijana wadogo wadogo, wakitutembelea, tunaona wana harufu kali za marashi, jambo ambalo halikuwa la kawaida zamani. Watengenezaji wa vipodozi wengi ni wanakemia wa kiume, zamani walikazana kutengenezea wanaume ila sasa upepo umebadilika. Huu ni uchaguzi, ila kwangu naogopa vitu vinavyoleta mvuto kwangu kupita kiasi, mapambo yanayofanya watu waache kufanya kila kitu wanitazame mimi, na sio kwamba inaniongezea usafi, au lolote, yabidi niyape pumziko kidogo.

Wanawake wengi wapenda kupendezesha waume zao, hivyo wanatumia vipodozi. Hapa mume amwambie mke wake vile ambavyo yeye anaona vyafaa au havifai. Marashi yale ya harufu kali ni ya kuepuka kutokana na allergy (mzio) na kuwapa watu chafya kila unapoenda. hata hivyo huvuta macho kwako na watu kukudhania visivyo kutokana na mazingira uliyopo, kwani ukipita harufu inabaki hewani na watu wengine watapata kipanda uso. Kuna hata sabuni nyingi za harufu kali zimeletea watu mzio. Sabuni ya kufulia ile ya ‘mti’ (mkaa au carbolic soap) brown ya mbuni au mkaa, yaonekana ni bora kwa wengi, kwa wale wenye shida ya mzio.

Hatuna historia ya vito ila Maandiko yameandika haya miaka zaidi ya 4000 iliyopita, ni vizuri kila mtu ayafanyie utafiti. Wakati wa Yakobo na wakati wa Musa wanaeleza baadhi ya mambo haya. “Basi wana wa Israel wakavua vyombo vyao vyote vya uzuri tangu mlima wa Horebu (Sinai) na mbele……..” Mungu aliumba vito, na tunafikiri alitaka tuvifurahie, ila visiwe kwa kujitukuza sisi. (haya ni maoni yetu tu).

Mapambo ya mwili, kutoboa sehemu za mwili ili kuweka vito yanaleta madhara ya ngozi kama kuvimba kwa masikio (keloids). Nabii Musa katika Torati (Walawi 19) kimezungumzia kidogo kuhusu tattoo au kujichora. Watu walishangaa wazee wa zamani waliojichora, kama Wamakonde kujichora na kuweka ndonya, hawa hawakuwa na uchaguzi. Leo mataifa ya magharibi yanaongoza katika biashara hii na wengine ukiona picha zao utakimbia. Yaonekana kama ni aina fulani ya ibada.

Kuna hoja nyingi dhidi ya kuvaa hereni au vito kwa ujumla hoja za afya, usalama, imani na hata usumbufu wa kila siku.

Wasiwasi wa Afya na Usalama: Watu wengi wana mzio wa chuma fulani hasa nikeli, ambayo hupatikana sana katika vito vya bei nafuu. Hii inaweza kusababisha ugonjwa wa ngozi na

kusababisha vipele vinavyowasha, vyekundu, au vinavyotoka usaha.

Maambukizi na Majeraha: Kutoboa shimo la hereni, au kipini, kunaweza kuleta maambukizo ikiwa hutasafishwa vizuri au ikiwa "tishu ngumu" kama gegedu imetobolewa. Pia kuna hatari ya kuumia kimwili, kama vile pete kung'olewa na mwizi au pete kukwama, ambayo inaweza kuhitaji kwenda hospitali.

Bakteria: Katika baadhi ya taaluma, kama vile huduma ya afya, vito vya mapambo havipendekezwi kwa sababu vinaweza kunasa bakteria na kufanya usafi wa mikono usiwe na ufanisi.

Xray na tiba: Vito vya mapambo vya chuma vinaweza kuingilia picha za X-ray na MRI kwa kuunda "picha za ajabu" au vitu vya kuficha maelezo muhimu ya uchunguzi.

Mitazamo ya Kidini na Kiroho

Ingawa baadhi ya vikundi vya kidini huruhusu vito vya mapambo, vinashauri waamini wao wasiweke vitu hivi:

Msisitizo juu ya Urembo wa Ndani: Baadhi ya madhehebu ya Kikristo hutaja 1 Petro 3:3-4 na 1 Timotheo 2:9-10, ambayo huwahimiza waumini kuzingatia mapambao ya moyo,  badala ya mapambo ya nje kama dhahabu au lulu.

Wasiwasi Kuhusu Kiburi na Ibada ya Sanamu: Vito vya mapambo wakati mwingine huonekana kama chanzo cha majivuno au "kujionyesha utajiri, kwa kiburi". Baadhi huelekeza kwenye masimulizi ya Biblia ambapo vito vilitumika kutengeneza sanamu, kama vile ndama wa dhahabu katika Kutoka 32.Ni bora ukadumisha umakini juu ya unyenyekevu na kuepuka masumbufu ya dunia.

Vikwazo vya Kutenda mema wa wahitaji

Gharama na Thamani: Vito vya mapambo vya ubora wa juu vinaweza kuwa ghali sana, na wengine wanasema pesa hizo zinaweza kutumika vyema kwingineko.

Matengenezo: Vito vya mapambo vinahitaji usafi wa mara kwa mara na utunzaji salama ili kuzuia uchafu, hasara, au wizi.

Kizuizi cha Kila Siku: Kwa baadhi, vito na mapambo huzuia shughuli za mikono unapofanya kazi kama kuosha vyombo, hutoa sauti zenye mlio wa kukasirisha au kuhisi vibaya wakati wa kulala au mazoezi.

Vipodozi vingine vyafanya ngozi iwe nyembamba na kuchanika kirahisi au kupata shida kushoneka mtu anapopata kidonda kikubwa. Vipodozi vingine vinachangia kuleta pumu au kikohozi kwa harufu yake, hata chunusi kwenye mwili. Vipodozi vyenye vichocheo vya wanawake vinaathiri vichocheo vya mtu (hormones) na kusababisha mzunguko wa hedhi wa wasichana uwe tofauti, au mabadiliko mengine mwilini. Vipodozi vingine vinavyotumika kwenye

kucha vyaweza kuwa na “Formaldehyde au toulene” ambazo ni dawa za kutunza maiti au nyama na hata kuleta madhara. Afya ya ngozi na kucha hutegemea sana chakula bora zaidi ya vipodozi. Madini kama ya chokaa, protein, vitamini A na B yahitajika kwa ajili ya kucha zetu.

**Je, wewe upo tayari kujikubali mwenyewe kama Mungu alivyokuumba?**

Kwa wale wanaotumia marashi (perfume) ni vyema yasiwe na harufu kali sana, hata yalete mzio wa kupiga chafya kwa watu au kwako. Mara nyingi kuna dawa za kupaka kwapani ambazo zinatoa harufu mbaya ya jasho (desdorant na siyo antipespirant) ila hazina harufu kali ya marashi, hizo ni nzuri. Ila zisikate jasho. Ila kila mtu ana uchaguzi wake. Kwa kifupi, kila kitu na kiasi, hasa ukipewa mahali pa wengi mfano kutoa houtuba, usiwe na marashi makali ukipita kupanda jukwaani, na watu wakasahau ujumbe wakifikiria haya marashi tu! Jaribu kuepuka mambo ya kukufanya wewe ndio uwe kiini. Ila usinuke jasho, nalo linapunguza mvuto. Najua kununua vya kukata jasho ni ghali, ila pengine angalia unavyoweza kutengeneza mwenyewe kama tulivyokwisha kusema.

Usafi wa kucha ni muhimu sana ili kusiwe na baktiria na kukuletea magonjwa. Zisafishe vizuri kwa sabuni, aloe vera au kitunguu saumu. Usikate kucha kwa meno, tumia ‘nail cutter’ au wembe. Tupa ya kucha (nail file) ni msaada pia wa kufanya zisivunjike-vunjike ovyo-nail. Usikwangue vocha za simu na kucha si afya. Ncha za kucha za miguuni zilowekwe zikiwa ngumu kukata, au zikate baada ya kuoga.

Tunarudia, Je, umeridhika na jinsi Mungu alivyokuumba? Wenzetu wazungu hawaonei aibu nywele au ngozi yao ila sisi tunataka kufanana na nao. Kuridhika na utauwa, ni jambo muhimu sana. Usijidhanie kama huna thamani mpaka ujiongezee mambo fulani, kama kujichubua ili uwe mweupe, kujiweka rangi, vipuli, n.k. Wote mara zingine tunajiona tumepelea ila tumwombe Mungu atusaidie tujithamini. Ikiwa Mwafrika ndiye angekuwa tajiri watu wote wangetaka kuja kuishi Afrika, na kuwa Waafrika, Mungu atusaidie kujitayarisha kwenda mbinguni, na kufanana Naye, na siyo kufanana na mtu mwenye ukomo, anayeishi bara fulani, na vito vyote vya platiki vitoke kwao, hii ina maana tunahitaji kucheua mada hii.

Kuna wengi ambao hawavai vito ila mavazi yao ni ya kujionyesha na ya ghali zaidi ya wale ambao wanavaa vito! Ila kitu kikubwa hapa ni kuwa na kiasi. Nimeona watu wanaovaa scarf ya dola 200 na wakisonda vidole vya mtu aliyevaa wigi ya dola 10! Na kusema wanaishi maisha ghali ya kujionyesha nje ya uwezo wao. Mwingine alinionyesha suti yake ya dola 5000, akadai ni rahisi wengine wana za dola 9000! Hapo mimi ningejenga nyumba ya vyumba saba!

Vipodozi vya kuweka kwapani ili jasho lisinuke vyabidi kutiliwa makini kwa vile vinaathiri mitoki. Jaribu kupata vipodozi vya kuweka makwapani ambavyo havina sumu. Vingi vina alminium ambayo ni sumu hivyo usipake. Kuna wengi wametengeneza vipodozi vyao peke yao kwa kutumia vitu vya asili. Google jinsi ya kutengeneza zako mwenyewe!

Mama mmoja aliniambia kwamba, shampoo ya kuoshea nywele anachukua siki vijiko viwili na baking powder vijiko viwili, chumvi na maji na inamsadia sana. Endelea kupeleleza vipodozi cha

kwapani visivyo na sumu, ila chumvi, mafuta ya nazi na baking soda ni viamba upishi vilivyotumia kwa karne kadhaa. Hakika chumvi-chumvi kama baking soda na vinegar unaweza kuanzia navyo kama viungo.

Soma kama krimu au mafuta ya nywele yana placenta, au vichocheo (hormones) vya wanawake na uepuke. Wanawake wa kimarekani weusi wametumia vitu hivi zaidi yetu, hivyo majaribio yao tuyasome maana ngozi yetu inafanana na yao, wamevitumia kwa miaka mingi. Wao wanajali sana mambo ya kuvaa na nywele, waliandika siku moja gazetini kwamba japo wapo asilimia ndogo, wanavaa 80% ya nguo zote Marekani! Sina uhakika kama ilikuwa wanawatania au kweli.

Yaliyoandikwa kuwa mfano kwenye utafiti wao ni: Wengi walipoteza nywele wakifikia utu uzima kwa permanent (perm), hivyo wana wanawake wengi wenye upara. Kansa ya matiti iko karibu mara mbili kuliko wanawake wa kizungu kwa sababu ya kutumia mafuta ya kukuza nywele ambayo yana vichocheo vya Kike vya toka kwenye kondo la mtoto anapozaliwa (oestrogen).

Unaweza kutengeneza sabuni na mafuta yako mwenyewe, ukiwa na nia. (Angalia kwenye YouTube, how to make your own soap). Sabuni nyingi za nje siku hizi zina allergy. Nimepewa na watu sabuni za uso za kutoka uchina wakisema za urembo! Nafikiri vitu vya namna hii ni vya kutumia kwa tahadhari. Uzuri anautoa Bwana, unapomjua anakubadilisha mtazamo wako! Kuna watu wenye uzuri niliokutana nao siku ya kwanza, walipoonyesha roho mbaya na ubinafsi baada ya muda akili yangu iliwafuta kwenye kitabu cha uzuri au urembo. Na wale ambao niliona hawapendezi siku ya kwanza baada ya muda niliona walikuwa kama Malaika, walipoonyesha huruma, kujali, na upendo kwa watu hata wasiowajua. Cindy rafiki yangu mzungu tulichukua naye madarasa alikuwa na sura nzuri, kupita wote darasani mwetu, ila alikuwa mgumu kufanya naye kazi au kusoma naye (complicated), mara hataki kukaa karibu na huyu, mara hataki kutumia kitabu pamoja na wengine, baada ya muda darasa zima walianza kumkimbia, uzuri wake ulichuja, na akapwaya. Kila ukimwona alikuwa peke yake. Tukumbuke mara nyingi vitu vya nchi nyingine havina viwango sana, na watu wanatuletea Afrika vile ambavyo havijapimwa au havijafikia viwango. Ila wanaogopa kuharibu soko na nchi za magharibi, hivyo wanapeleka huko vitu vizuri tu. Mfano mzuri ni dawa za uzazi wa majira, ambazo zimeua wengi katika nchi nyingi kama zile njiti waliweka kwenye mkono kwa miaka 5 (Nexplanon).

Aliimba mtunga nyimbo Tanzania, "Sisi waafrika tumekosa nini kwa Mungu, chochote kibaya ni cha mwafrika!" Aliniambia kaka yangu, "Kama kuna mtu inabidi akazane aende mbinguni ni Mwafrika kwani tumeonewa, tumenyanyaswa na kudharauliwa kwa utumwa, ukoloni, madikteta, umasikini na ukoloni mamboleo, na kama tukikosa mbingu basi tutakuwa tumekosa ya hapa duniani na huko mbinguni!" Kwa ujumla fanya mambo yako yawe rahisi hata mafuta ya kujipaka, hakuna mazuri kama yale ya chakula. Tumia mafuta ya chakula kujipaka, ongeza tu marashi ya asili kama unataka kufanya hivyo. Jithamini, maana umeumbwa na kununuliwa kwa thamani kubwa na Mungu Mwenyewe (created and redeemed).

Usiwe mtu wa kujionyesha au uliye nyuma sana, ukivaa vitu ambavyo haviko kwenye ratiba tena

bali vya vichekesho, au usiwe mbele sana na kuwa mtu ambaye unaendana na fasheni mno. Hata hivyo tuna bahati kwamba kuna nguo ambazo ni nzuri kwa wakati wote (evergreen). Zenyewe hazina fashion kama vile maxi, sketi za mwamvuli nk. Nafikiri wanaume wengi watakubaliana kwamba wao nguo zao nyingi hazina shida ya fasheni, ikiwa ni suti nadhifu yaweza kuvaliwa miaka nenda rudi, ukipiga viatu vyako rangi basi maisha yanaendelea.

SISI NI MABALOZI na MAWAKILI wa MUNGU-Je,

Kwanini Tunavaa Nguo? Je, ni vibaya wanawake kuvaa suruali? Je, Mavazi ya heshima ni Yapi? Kwanini Wakristo wana mavazi ya kukosa adabu kuliko Waislamu?

Jipatie kitabu cha Mavazi kwa muumini, bure, soft copy

## Je, MWANAMKE AVAE SURUALI?

Kuhusiana na Mavazi ya zamani ya watu wa Biblia, wanaume na wanawake walivaa majoho, na ndani waliweka suruali au kaptura ndefu. Mavazi ya Haruni ni mfano unaopaswa kujifunzwa, maana kuna kile MUNGU alimwambia avae kwa kujistahi na kumheshimu Mungu hata katika miaka ya 1800. Vazi lililopendekezwa lilikuwa na suraali ndani na kufanana na vazi la wahindi liitwalo Punjabi. Kwa vile leo suruali ni vazi la mwanamume ni vyema mwanamke asivae vazi hili kutokana na utamaduni wa dunia hii. Hata hivyo kuvaa suruali yenyewe bila ya blausi isiyobana inayofika chini na kufunika matako kutokana na maumbile ya mwanamke inamfanya mwanamke ajionyeshe kuwa hajavaa kwa kujisitiri au heshima.

Hivyo kwa mwanamke anayevaa suruali ni vyema ajue jinsi yakuvaa blauzi refu kama ya aina ya Panjabi

wanavyovaa wahindi au ile ambayo isiyobana na inafunika matako.

Sasa mambo haya ni endelevu kadri tunavyomjua Mungu na jinsi mitindo inavyoingia, hatupaswi kuparamia kila kitu na kuwa wa kwanza katika mambo ya fasheni. Watoto wasichana wadogo pia wafundishwe haya wakiwa wadogo, jinsi wanavyopaswa kuketi hata wakiwa kwenye mimbari nk, wasikae katika mimbari wakati wakihudumu au wakisimuliwa visa vya Biblia huku nguo za ndani zinaonekana, au wanajaribu

kuvuta-vuta nguo ili zifike magotini. Nguo inapaswa kufika angalau chini kidogo ya magoti, wakati mtu amesimama au amekaa.Watoto  pia nao wanapaswa kuvalishwa kaptura ndani ya magauni yao kwa vile wanacheza na kama watoto hawawezi kuangalia mambo mengine. Naweza kusema hata kwa watu wazima wengi kuvaa kaptura au suruali ndani ya gauni husaidia katika kuinama na kufanya kazi fulani, endapo gauni halimsitiri mtu vizuri, Kuhusu nguo za kuogelea watu wengi wana nguo za kuogelea za heshima, nimekutana na wasichana wa Kiarabu wanaogelea na wamevaa mavazi ya adabu tu, hatuna haja ya kuigiza utamaduni wa magharibi, hakuna haja ya kujionyesha kwa wengine kwa kuvaa vichupi vidogo na visidiria.

Ila napenda kusema kwamba kuvaa suruali yaweza kuwa jambo la lazima kwenye sehemu za baridi. Yaani Wakati wa Baridi kali. Mfano kwetu wakati wa baridi

ni -26 Centigrade. Hii ni baridi kali, wakati kama huu ninavaa suruali mbili au hata tatu. Sururali ya kwanza inakuwa ya fulana, ya pili ya kawaida na ya tatu ya khaki au jeans ili kujikinga na upepo. kisha navaa blausi moja ya fulana ndani na gauni, kisha sweta la fulana lenye kofia (sweater with the hood) na kisha koti zito kabisa juu. Nikitoka nje kufanya kazi sitoki kwa kukurupuka, ni lazima nitumie ubongo, niliambiwa na wazazi wangu wa Kimarekani Dr and Mrs Wilson Trickett "tumia ubongo wako kulinda miguu yako! Au sehemu zako za mwili zilizo mbali na moyo kama vile miguu, mikono na kichwa"

Kingereza alisema "Use your head to protect your legs, au protect your extremities, or your limbs" Kadri kulivyo na tabaka/layers nyingi za nguo mwilini, ndiyo unajikinga na baridi zaidi. Kisha navaa jozi tatu za soksi, na kisha buti za winter zenye manyoya ndani yake. Kisha navaa gloves pamoja na kofia chini ya koti lenye kofia/ hivyo nakuwa na kofia mbili au tatu.

Kofia ya kwanza ni ile ya sweta la fulana, ya pili ni ya sweta inaenda yenyewe na ya tatu ni ile ya koti zito.

Kusema kwamba nitatembea na gauni bila ya suruali ni kujitakia shida, na hasa wakati huu wa Korona, mapafu yatapata shida, na hutaweza kufanya kazi nje. Kama sasa inabidi kukata kuni za kufanya nyumba iwe na joto wakati wa baridi, inabidi nitembee mazoezi angalau saa moja kila siku, na navyoshugulikia kuhariri machapisho kila baada ya saa au masaa mawili natoka nje. Ukiwa na mtoto mdogo unapojipanga kutoka naye au kwenda kanisani, lazima ujipange vizuri naye na kisha umvishe layers/tabaka kadhaa ya nguo za kuleta jozi. Mikono, kichwa na miguu yetu lazima ilindwe maana ipo mbali na moyo hivyo kusafiri kwa damu kunachukua muda.

Tusiseme tu kwamba mtu asivae Suruali lazima mtu tueleze sababu, kwasababu kwenye Biblia suruali haikuwa vazi la nje la mwanamke au mwanamume.

Hakuna mwanamume au mwanamke aliyevaa suruali yenyewe katika Maandiko! Mwanamke anayevaa suruali

yenye blauzi inayofunika vizuri anajistahi kuliko aliyevaa gauni linaloonyesha mgongo, mapaja kwaajili ya sliti au hata makwapa, na sehemu za mwili kwa vile linabana au lina kitambaa kinachoonyesha mwili ndani au matiti,  Katika mishono ya vazi la kitaifa, ni jambo ambalo ni la kawaida kabisa kwenye mishono mingi ya

kitaifa kuacha mgongo au kifua wazi au kupasua nguo kwa mtindo unaoitwa slit. Hivyo ni bora mtu akavaa Suruali na kujisitiri kama vile wahindi wanavyovaa na blauzi refu, kuliko sisi tunavyovaa.

Nafikiri utamaduni wetu kwa ajili ya kanga na kaniki umetufanya kuzoea kuacha kifua au mgongo wazi. Ila kama tulivyosema huko mbele mtu anayepaswa kuona uchi wa mtu mwingine ni mzazi wa mtoto mdogo, mwenzi wa mtu aliye naye kwenye ndoa, Daktari kwaajili ya tiba na yule anayesafisha maiti, kituo kikubwa. Ila katika enzi zote au tuseme ujana watu huwa tunashikwa na ugonjwa wa kujionyesha ambao unakwisha mtu akiwa mtu mzima, ila mtu anayeishindania imani waliyopewa Watakatifu, ugonjwa huu haupaswi kumshika akiwa msichana au mama wa miaka 100!

Hebu turudi kwenye kichujio kile kile cha Wafilipi 4:8

"Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya Kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo."

Kwa maneno mengine tumwombe Mungu atupe moyo uliovunjika na kupondeka, hatuwezi kuwa watu wenye shingo ngumu. Hatutaki tuwakwaze watu, lakini hata hivyo

tukumbuke kuna tamaduni mbali mbali za mavazi tofauti na katika tamaduni zile ambazo watu hawakuvaa kwa heshima wanapomwamini Mungu wanabidi wabadilike na wavae kwa heshima ila sisi hatutakuwa mapolisi wao kuangalia hayo saa yote, kwani hata shuguli zetu tutazifanya saa ngapi? Maana unaweza kuvaa kwa kujifunika kila mahali ila pengine una maisha ya urafiki mbaya

**na wanaume au wanawake kwa siri. Unaweza kuwa unenda huko ukiwa umevaa ushungi na unalala huko na kufanya mengi, kama vile kuchukua waume wa watu, kufanya njama za kuua watu au kusengenya. Je itasaidia nini basi kama umevaa nguo inayoburuza chini na ushungi ila umejaa uovu moyoni na kuwa na hiana? Naomba nawe utoe maoni yako, maana hapa nasema kama mwanadamu!**

Watoto wa mama mdogo Hajiri huvalia kwa adabu kuliko sisi watoto wa mama mkubwa Sarai, sababu ni ipi basi,

nasi tuna ujumbe wa Masihi ambaye Anakuja hivi karibuni? Japo kitabu hiki kimezungumzia fasheni au mitindo ya miaka 150 iliyopita, inabidi tulinganishe na maisha yetu leo, na kuona pale tunapopaswa kufanya matengenezo ya mavazi ili kuendana na vile Mwenyezi Mungu anataka, na siyo sisi.

Maandiko Matakatifu hayana mambo ya zamani! Maagizo Yake ni ya milele! Kigezo kikubwa ni tulapo au tunywapo au tufanyapo japo lolote, tulifanye kwa Utukufu wa Mungu.

Rejelea yale mashauri pale juu kwamba “Hakuna mtu yeyote anayepaswa kuuona utupu wetu ila mzazi mtoto anapokuwa mdogo, mtu tuliye naye katika ndoa, daktari kwa ajili ya tiba, na yule anayeosha mwili wakati wa kuzika kaburini,” fullstop, kituo kikubwa.

Yaani tunaponunua nguo, tunapovaa asubuhi, tuwaze je, navaa leo ili kumtukuza Mungu, au kuwatukuza madizaina au kujionyesha kwa watu? Hakuna asiyepungukiwa hapa maana sote tunataka watu watuone tunapovaa! Hilo ndiyo jambo la kweli kabisa . Na hilo ni muhimu ili tusivae magunia au nguo

kama za kufukuzia ndege mashambani, nayo pia haitampa Mungu utukufu. Uwiano (balansi), Mungu atatusaidia!

Hakuna mwenye uwezo huo isipokuwa YEYE tu!

Wapendwa kitabu hiki ni chetu sote! Maana Masihi Anakuja kuchukua bibi harusi asiye na waa wala kunyanzi. Maneno haya yametuchoma sana, na yanatushawishi tusiwe waongofu tu bali wanafunzi na watu wanaoishi kwa uamsho na matengenezo kila siku, tukiendelea kuwezeshwa na Roho Mtakatifu kubadilisha mitindo yetu ya maisha ili tumpende na kumpendeza Mwenyezi MUNGU, na kuwapenda watu. Katika kukitafsiri tuligundua kwamba utamaduni na enzi za vazi la Matengenezo, inaweza isieleweke vyema na watu wa taifa letu, na hivyo nukuu zingine baada ya kitabu inabidi kurejelewa na picha kuwekwa ili mtu aelewe angalau kwa udogo kile ambacho kilikuwa kikiendelea.

Tumeitwa kumwakilisha Mungu katika maneno, matendo, kula, na kuvaa, ili watu wamwone na kumfuata Yeye, na si sisi wenyewe. Tukimpenda Mungu hatutabaki kama tulivyo kani tutabadilishwa siku kwa siku kwa kumtazama Yeye, tutafanana Naye. Kamwe hatutaabudu mitindo, mavazi, mapambo au chochote zaidi ya Mwenyezi Mungu.

Tumesoma mafungu mengi kwenye Maandiko kama vile “Siku hiyo kila mtu atazitupilia mbali sanamu zake za fedha, na sanamu zake za dhahabu, walizojifanyia ili kuziabudu, kwa fuko na popo”-Isaya 2:20 au “ Bwana akasema tena, Kwa sababu binti za Sayuni wana kiburi, na kuenenda na shingo zilizonyoshwa, na macho ya kutamani, wakienenda kwa hatua za madaha, na kuliza njuga kwa miguu yao; Basi, kwa hiyo, Bwana atawapiga binti za

Sayuni kwa pele za utosini, na Bwana ataifunua aibu yao. Siku hiyo Bwana atawaondolea uzuri wa njuga zao, na kaya zao; na pete za masikio, na vikuku, na taji zao; na dusumali, na mafurungu, na vitambi, na vibweta vya marashi, na matalasimu; na pete, na azama, na mavazi ya sikukuu, na debwani; na shali, na vifuko; na vioo vidogo, na kitani nzuri, na vilemba, na utaji. Hata itakuwa ya kuwa badala ya manukato mazuri kutakuwa uvundo, na badala ya mishipi, kamba; na badala ya nywele zilizosukwa vizuri, upaa; na badala ya kisibau, mavazi ya kigunia; na kutiwa alama mwilini kwa moto badala ya uzuri."Isaya 3:16-21. au Kujipamba kwenu, kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi; bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu. Maana hivyo ndivyo walivyojipamba wanawake watakatifu wa zamani, waliomtumaini Mungu, na kuwatii waume zao. Kama vile Sara alivyomtii Ibrahimu, akamwita Bwana; nanyi ni watoto wake, mfanyapo mema, wala hamkutishwa kwa hofu yoyote. 1 Pet 3:3-6

Nguvu ya injili hutoka ndani ya moyo ndiyo humbadilisha mtu, nayo ni endelevu kadri tunavyoendelea kukua katika

Kristo, vitu vingine mtu hawezi kutuambia bali tutajikuta tunaviacha wenyewe kwa furaha bila hata ya kubishana na mtu, kwani tutagundua kuwa tunaokolewa kwa neema na si kwa mavazi au mapambo yetu. Ni vigumu kumwekea mtu kigezo, na akakifuata kwa moyo wake wote. Ni kawaida ya binadamu kujionyesha na kutaka watu wamwangalie ili kuona uzuri wake, elimu, ujuaji, utajiri wake nk. Hivi vyote vinaturudisha nyuma kiroho kwani kwa desturi, huwa tunapenda kuabudu nafsi zetu, tupende au tusipende kulimeza hili, huu ndio ukweli wenyewe ulivyo.  Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anatuagiza watu wote wa kila mahali tutubu. Kwa maana ameweka siku atakayotuhukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; Naye ametupa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua Yesu katika wafu Matendo 17:30, 31. Tunaishi wakati wa maarifa mengi, na Maandiko Matakatifu ndiyo kitabu kinachouzika duniani kuliko kitabu kingine kwa miaka takribani miaka 3000 hivi, toka Musa alipoandika na watu wakanakili kwa mkono na hata watu wa dini za mashariki wametuonyesha, mishono ya mavazi ambayo sisi tulio Wakristo tunapaswa kuyatilia makini, ili tusimwaibishe Mungu.

Mara nyingi tunapozungumzia uwakili, huwa tunasema uwakili wa muda, fedha, afya nk, ila uwakili ni mitindo yetu ya maisha, ni jumla ya mambo yote. Uwakili ni kufanana na Kristo, kuiga tabia Yake (emulate Him), Wema Wake, kuilinda injili ambayo tumepewa sisi ambao

ni vyombo vya udongo.

## KWANINI TUNAVAA NGUO?

Sababu peke yake ya sisi kuvaa nguo ni MWENYEZI MUNGU alituambia baada ya dhambi, kwamba “sasa Mimi sikuviki na utukufu Wangu, hebu ufiche aibu yako, Sisi si mapolisi wa dunia wa kuwaambia watu wavae nini, vito gani wanapaswa kuviweka, wale nini, wazungumzaje, waimbe nyimbo zao namna gani, au wakae nyumba ya namna gani etc

**KICHUJIO CHETU** wote wenye mwili ni Kile Mungu amekitoa baada ya maagizo YAKE, yaani kile cha Wafilipi-4:8
Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo ya staha, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote yenye kupendeza, yoyote yenye sifa njema; ukiwapo wema wowote, ikiwapo sifa nzuri yoyote, yatafakarini hayo.
9 Mambo mliyojifunza kwangu na kuyapokea, na kuyasikia na kuyaona kwangu, yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi." Haruni kama mwanamume aliambiwa atakapopanda ngazi kwenye madhabahu ya kukutania avae kaptura ndani, mapaja yake yasionekane, asije akakatiliwa mbali. Hiki kinaonyesha kwa wale waliotambulishwa Kidogo kwenye Maandiko kama sisi, tumeanza safari endelevu ya kuchuja mambo mengi kwa uwezo wa Mungu kupitia, upendo, Maandiko, maombi, Roho Mtakatifu, hekima, na uzoefu bora. Hakuna kesi zinazofanana-fanana, sisi si mapolisi wa wengine ila pia sisi si mbwa wasiobweka! Tutajuaje tofauti? Kwa kuomba, na

upendo kwa watu hawa. Hatuwezi kuwakenulia meno kama watapata shida, na hatuwezi kuwa polisi wao. Tunachoomba ni hekima tu kutoka kwa Mungu katika kila hali tunayokutana nayo, tunahitaji Mshauri wa Ajabu. MUNGU atusaidie kujibadilisha sisi wenyewe zaidi ya mtu yoyote!

Maana tunawajibika kwetu wenyewe zaidi ya kwa mtu mwingine. Ila watu tunaofanya nao urafiki, tukiwashauri kwa upendo tunapoona wanahitaji ushauri, litakuwa jambo bora. Ila inakuwa rahisi zaidi kumshauri mtu ambaye ni rafiki. Usigombane na watu, fanya haya kwa upendo, maana unaweza ukashinda vita ila upoteze roho, au ukashinda pambano, ila ukashindwa vita.

Ezekieli 3 Yasema, Akaniambia, Mwanadamu, haya! Waendee wana wa Israeli ukawaambie Maneno Yangu. Maana wewe hukutumwa kwa watu wa maneno mageni, ama wa lugha ngumu, bali kwa nyumba ya Israeli; si kwa watu wa kabila nyingi wenye maneno mageni, na lugha ngumu, ambao huwezi kufahamu maneno yao. Bila shaka, kama ningekutuma kwa watu hao, wangekusikiliza. Bali nyumba ya Israeli hawatakusikiliza wewe; kwa kuwa hawanisikilizi Mimi; maana nyumba yote ya Israeli wana vipaji vigumu, na mioyo yenye ukaidi. Tazama, nimeufanya uso wako kuwa mgumu juu ya nyuso zao, na kipaji cha uso chako kuwa kigumu juu ya vipaji vya nyuso vyao.

Sasa tujiulize kama vitu hivi ni vya muhimu sana kwetu? Kila mtu anapaswa kuchunguza moyo wake na kuonya vile anavyopaswa kuviacha au kusahihisha. Sisi hatuna kipimo yaani Spiritualmeter au Christometer, ila kwa mambo machache tumepewa kazi ya kukagua matunda ila tusipende kuyakagua matunda saa zote Mathayo 7:15-20

Ni vyema tuseme kuwa katika enzi zote au pengine tuseme ujanani, watu hushikwa na ugonjwa wa kujionyesha ambao unakwisha mtu anapofikia utu uzima, ila mtu anayeishindania imani waliyopewa Watakatifu, ugonjwa huu haupaswi kumshika akiwa msichana au mama wa miaka 100!

Mungu awabariki mnaposoma kitabu hiki, kwani hakuna mwanadamu mwenye jibu la kila swali, ila tukitumia vigezo vilivyoandikwa mwenye kitabu hiki, hakika hatutafeli. Nasi siku moja tutavikwa taji na vito vyenye thamani, na Yule aliye wa Thamani Kupita vyote mbinguni na duniani, Ndilo ombi langu

Masihi Anarudi. Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo.Amina. Njoo Bwana Yesu!Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. MARANATHA Wapendwa wa

BWANA! Amina

**Tembelea -MAARIFAmtandaoni.Com au RohoYaUnabii.Org**

Unafikiri ni vitabu gani viandikwe ili kusaidia au kutafsiriwa, tupe mapendekezo yako

***Vitabu vya Kalamu ya Uvuvio vilivyotafsiriwa or self help books***

**THE FOLLOWING ARE BOOKS TRANSLATED or Written in SWAHILI**

1.Testimonies for the church 9 Volumes
10.Fundamentals of Christian Education
11.Pastoral Ministry
12.*The Great Controversy*
13.Counsel for the Church
14.Heaven
15.About the Angels
16.Testimonies on Sexual Behaviour, Adultery and Divorce
17.Welfare Ministry
18. Prayer
19. Short Version of Prayer
20. Gospel Workers
21. Campmeetings
22. Dress Reform
23. Mission to the Cities
24. Steps to Christ
25. Food Ministry
26. Story of Redemption
27. *Early Writings*
28. Ministry of Healing
29. Story of Redemption
30. Counsels to Teachers, Parents and Students
31. Testimonies to Ministers and 'Gospel Workers
32.Counsel in Diet and Foods-not edited

33.Early Writings
34.God's Remnant Church
35. Counsel on Health
36. Retirement Years
37. Peter's Counsel-not edited
38. Evangelism
39. *Child Guidance*
40. Adventist Home
41. Medical ministry-not edited
42. an Appeal to mothers-not edited
43. Manuscript Release Volume 1
44. The Southern Work
45 Selected Messages volume 1
46. Selected Messages Volume 2
47. Bible Commentary Volume 7a
48. Broke Blue Print
49. Medical Missionary Manual
50. Greek Strong-New Testament-Old is being done now
51. Desire of Ages
52. Tell it to the world-uambie ulimwengu
53. Path to the throne on pipeline
54. People of Providence

**Books Written**

2.Children Bible in form of 365 Devotion Swahili and English
Biblia ya watoto-Visa 407 vya Biblia katika mfumo wa Kesha
4.Layman-Mlei Swahili and Englishi
5.21st Century godly woman Mwanamke wa Karne ya 21
5.Summary of the Bible-Muhtasari wa Biblia still on editing, has not come yet
6. DO HARD THINGS-FANYA VITU VIGUMU appeal for youth-by harris translation
7. Your Health-What should you do? Jinsi ya kusaidia afya yako-English and Swahili
9. Parenting-Kuzaa na Kulea, Swahili and English
10 . 42 percent of people have not been reached
11. Teaching Children, youth and adults about issues pertaining to sexuality
12. Three angels messages
13. Mambo ya kuombea watoto wako
14. Biblia ya Ahadi na Maandishi mekundu pale Mungu/KRISTO WANAZUNGUMZA
15. BIBLIA YA KRONOLOJIA
16. NGUVU YA UKARIMU HOSPITALITY
17. NGUVU YA KUOMBEA NA KUBARIKI WATOTO WAKO

18. NATURAL HEALTH BY JAMES LUKE AND NATASHA OF TRINIDAD-TRANSLATION
19. DO HARD THINGS-FANYA VITU VIGUMU appeal for youth-by harris translation
20. Courtship 100 questions to ask and also distillation of courtship documentary on pipeline

21. Teaching a child to read Swahili

Ufafanuzi wa vitabu 66 vya Biblia kwa Kiswahili-Na majadiliano
COMMENTS ON 66 BOOKS OF THE BIBLE-ABOUT 16,000 PAGES-EACH BOOK WILL BE SEPARATED, SWAHILI AND ENGLISH

# 222 Maombi ya Biblia

Kuna maombi zaidi ya 222 kwenye Biblia, 176 katika Agano la Kale na 46 katika Agano Jipya.Maombi halisi, wala sio marejeo ya sala. Kauli zote "alipoomba, akamwomba Bwana, akaliitia Jina la Bwana,".

Unabii 351 wa Agano la Kale Uliotimizwa Katika Yesu Kristo

Unabii--------------

Maelezo-----------

Utimilifu-----------

**Mifano ya Yesu**

Mifano ya viriba vipya na ngozi mpya za Divai

Mfano wa Kinara cha Taa

Mfano wa mjenzi mwenye Hekima na mpumbavu

Mfano wa Mpanzi

Mfano wa Magugu

Mfano wa Mbegu ya Haradali

Mfano wa Chachu

Mifano ya Hazina Iliyofichwa na Lulu

Mfano wa Nyavu

Mfano wa Mwenye Nyumba

Mfano wa Kondoo Anayetangatanga

Mfano wa Mtumishi Asiye na Rehema

Mfano wa Wafanyakazi katika Shamba la Mizabibu

Mfano wa Wana Wawili

Mfano wa Wapangaji

Mfano wa Karamu ya Harusi

Mfano wa Mtini

Mfano wa Wanawali Kumi

Mfano wa Talanta

Mfano wa Kondoo na Mbuzi

Mifano ya Marko

Mfano wa Mbegu Inayoota

Mfano wa Mmiliki Anayerudi

Mifano ya Luka

Mfano wa Mkopeshaji Pesa

Mfano wa Tajiri Mpumbavu

Mfano wa Watumishi Walio Macho

Mfano wa Watumishi Wenye Hekima na Wapumbavu

Mfano wa Mtini Usiozaa

Mfano wa Bwana na Mtumishi

Mfano wa Msamaria Mwema

Mfano wa Rafiki anayetafuta Mkate

Mfano wa Mahali pa Heshima

Mfano wa Karamu Kubwa

Mifano kuhusu Kuhesabu Gharama

Mfano wa Kondoo Aliyepotea

Mfano wa Sarafu Iliyopotea

Mfano wa Mwana Mpotevu

Mfano wa Meneja Mwerevu

Mfano wa Tajiri na Lazaro

Mfano wa Mjane Mvumilivu

## Miujiza ya Yesu

1. Kubadilisha maji kuwa divai (Yohana 2:1-11)

2. Kufanya ishara Yerusalemu (Yohana 2:13-25)

3. Kuponywa kwa mwana wa afisa wa kifalme (Yohana 4:46-54)

4. Kuvua samaki wengi (Luka 5:3-10)

5. Kuponywa kwa mtu aliyekuwa na pepo huko Kapernaumu (Marko 1:21-28, Luka 4:33-37)

6. Kuponywa kwa mama mkwe wa Simoni Petro (Mathayo 8:14-15, Marko 1:29-31, Luka 4:38-39)

7. Kuponya wagonjwa wakati wa jioni (Mathayo 8:16, Marko 1:32, Luka 4:40)

8. Kumponya mwenye ukoma (Mathayo 8:1-4; Marko 1:40-45; Luka 5:12-15)

9. Kumponya mtu aliyepooza (Mathayo 9:1-8, Marko 2:1-12, Luka 5:18-26)

10. Kumponya mtu aliyekuwa kiwete kwa miaka 38, kwenye Bwawa la Bethzatha (Yohana 5:1-18)

11. Kuponya mkono uliopooza (Mathayo 12:9-14, Marko 3:1-6, Luka 6:6-10)

12. Kuponya watu kwenye umati uliomfuata Galilaya (Mathayo 12:14-21, Marko 3:6-12)

13. Kuponya watu wengi kabla ya kutoa mahubiri Galilaya (Luka 6:17-19)

14. Kumponya mtumishi wa akida (Mathayo 8:5-13, Luka 7:1-10)

15. Kumfufua mwana wa mjane huko Naini (Luka 7:11-17)

16. Kuponya watu wakati wa ziara ya wanafunzi wa Yohana Mbatizaji (Luka 7:18-35)

17. Kumponya mtu kipofu na bubu mwenye pepo (Mathayo 12:22-37)

18. Kutuliza bahari yenye dhoruba (Mathayo 8:23-27, Marko 4:35-41, Luka 8:22-25)

19. Kumponya mtu aliyekuwa amepagawa na pepo wa Gerasa (Mathayo 8:28-32, Marko 5:1-13, Luka 8:26-33)

20. Kumponya mwanamke aliyetokwa na damu ndani (Mathayo 9:20-22, Marko 5:25-34, Luka 8:43-48)

21. Kumfufua binti wa Yairo (Mathayo 9:18-19, 23-25; Marko 5:22-24, 35-43; Luka 8:41-42, 49-56)

22. Kumponya vipofu wawili (Mathayo 9:27-31)

23. Kumponya mtu bubu aliyekuwa amepagawa na pepo wachafu (Mathayo 9:32-33)

24. Yesu anawaponya watu wachache baada ya kukataliwa Nazareti (Mathayo 13:53-58, Marko 6:1-6)

25. Yesu anawapa mitume Wake uwezo wa kufanya miujiza (Mathayo 10:1-8, Marko 6:7-13, Luka 9:1-6)

26. Uponyaji wa wengi huko Bethsaida (Mathayo 14:13-14 na Luka 9:10-11)

27. Kuwalisha wanaume 5000 na familia zao (Mathayo 14:16-21, Marko 6:35-44, Luka 9:12-17, Yohana 6:5-14)

28. Yesu anatembea juu ya maji (Mathayo 14:22-33, Marko 6:45-52, Yohana 6:16-21)

29. Uponyaji wa wengi huko Genesareti (Mathayo 14:34-36; Marko 6:53-56)

30. Kumponya binti wa mwanamke Mkanaani aliyekuwa amepagawa na pepo (Mathayo 15:21-28, Marko 7:24-30)

31. Kumponya kiziwi asiyeweza kusema (Marko 7:31-37)

32. Kuponya watu wengi katika na karibu na Dekapoli (Mathayo 15:29-31)

33. Kuwalisha wanaume 4000 na familia zao (Mathayo 15:29-39, Marko 8:1-10)

34. Kumponya kipofu huko Bethsaida (Marko 8:22-26)

35. Kumponya mvulana mwenye pepo (Mathayo 17:14-20, Marko 9:17-29, Luka 9:37-43)

36. Kuvua samaki akiwa na sarafu kinywani mwake (Mathayo 17:24-27)

37. Kumponya mtu aliyezaliwa kipofu huko Yerusalemu (Yohana 9:1-41)

38. Yesu anawapa mitume Wake nguvu za miujiza (Luka 10:1-17)

39. Kumponya bubu Mwanamume aliyekuwa amepagawa na pepo (Luka 11:14-28)

40. Kumponya mwanamke mwenye ulemavu wa miaka 18 (Luka 13:10-13)

41. Kumponya mtu mwenye ugonjwa wa kupooza (Luka 14:1-6)

42. Kumfufua Lazaro (Yohana 11:1-44)

43. Kuponya wanaume 10 waliokuwa na ukoma (Luka 17:11-19)

44. Kumponya Bartimayo mwenye upofu (Mathayo 20:29-34, Marko 10:46-52, Luka 18:35-43.

45. Kuponya vipofu na viwete Hekaluni (Mathayo 21:12-17)

46. Mtini unaonyauka ambao haukuzaa matunda (Mathayo 21:18-22; Marko 11:12-14, 20-25)

47. Kurejesha sikio lililokatwa (Luka 22:45-54)

48. Yesu anawatokea mitume Wake baada ya kufufuka (Yohana 20:19-21)

49. Yesu anamtokea Tomaso baada ya kufufuka (Yohana 20:24-28)

50. Kuvua samaki 153 (Yohana 21:4-11)

---

# 222 Maombi ya Biblia

Kuna maombi zaidi ya 222 kwenye Biblia, 176 katika Agano la Kale na 46 katika Agano Jipya.Maombi halisi, wala sio marejeo ya sala. Kauli zote “alipoomba, akamwomba Bwana, akaliitia Jina la Bwana,”

---

Unabii 351 wa Agano la Kale Uliotimizwa Katika Yesu Krist

Unabii--------------

Maelezo-----------

Utimilifu-----------

1. Mwa 3:15  -Uzao wa mwanamke (kuzaliwa na bikira)- Wagalatia 4:4-5; Mathayo 1:18

2. Mwa 3:15 -Atamponda kichwa Shetani- Waebrania 2:14; 1 Yohana 3:8

3. Mwa 5:24- Kupaa mbinguni kimwili kulionyeshwa- Marko 16:19

4. Mwa 9:26-27- Mungu wa Shemu atakuwa Mwana wa Shemu- Luka 3:36

5. Mwa 12:3 -Uzao wa Ibrahimu utabariki mataifa yote-Wagalatia 3:8; Matendo 3:25-26

6. Mwa 12:7- Ahadi Iliyotolewa kwa Uzao wa Ibrahimu- Wagalatia 3:16

7. Mwa 14:18- Kuhani kwa mfano wa Melkizedeki -Waebrania 6:20

8. Mwa 14:18- Mfalme wa Amani na Haki- Waebrania 7:2

9. Mwa 14:18- Karamu ya Mwisho ilitabiri- Mathayo 26:26-29

10. Mwa 17:19 -Uzao wa Isaka (Mwa 21:12)- Warumi 9:7

11. Mwa 22:8 -Mwana-Kondoo wa Mungu aliyeahidiwa- Yohana 1:29

12. Mwa 22:18 -Kama uzao wa Isaka, atabariki mataifa yote- Wagalatia 3:16

13. Mwa 26:2-5- Uzao wa Isaka ulioahidiwa kama Mkomboz-i Waebrania 11:18

14. Mwa 28:12- Daraja la kwenda mbinguni -Yohana 1:51

15. Mwa 28:14- Uzao wa Yakobo -Luka 3:34

16. Mwa 49:10 -Wakati wa kuja Kwake- Luka 2:1-7; Gal 4:4

17. Mwa 49:10- Uzao wa Yuda- Luka 3:33

18. Mwa 49:10- Aliyeitwa Shilo au Aliyetumwa- Yohana 17:3

19. Mwa 49:10 -Masihiaja kutoka kabila ya Yuda kupoteza utambulisho- Yohana 11:47-52

20. Mwa 49:10- Utii wa watu utakuwa Kwake- Yohana 10:16

21. Kutoka 3:13-15- "MIMI NIKO" Mkuu-Yohana 4:26; 8:58

22. Kutoka 12:5 -Mwana-Kondoo asiye na dosari -Ebr 9:14; 1 Pet 1:19

23. Kutoka 12:13- Damu ya Mwana-Kondoo huokoa kutoka kwa ghadhabu -Rum 5:8

24. Kutoka 12:21-27- Kristo Ndiye Pasaka yetu- 1 Kor 5:7

25. Kutoka 12:46- Hakuna mfupa wa Mwana-Kondoo utakaovunjwa -Yohana 19:31-36

26. Kutoka 15:2 -Kuinuliwa Kwake kulitabiriwa kama Yeshua -Matendo 7:55-56

27. Kutoka 15:11- Tabia Yake-Utakatifu- Luka 1:35; Matendo 4:27

28. Kutoka 17:6 -Mwamba wa Kiroho wa Israeli- 1 Kor 10:4

29. Kutoka 33:19- Tabia Yake-Mtu Mwenye Huruma -Luka 1:72

30. Mambo ya Walawi 1:2-9- Sadaka Yake yenye harufu nzuri kwa Mungu- Efe 5:2

31. Mambo ya Walawi 14:11- Mwenye ukoma kusafishwa-Ishara ya ukuhani- Luka 5:12-14; Matendo 6:7

32. Law 16:15-17- Atakufa kifo cha mara moja cha Kristo, siyo kama dhabihu kila siku- Ebr 9:7-14

33. Law 16:27- Atateseka nje ya Kamb-i Mathayo 27:33; Ebr. 13:11-12

34. Law 17:11 -Damu - uhai wa mwili- Mathayo 26:28; Marko 10:45

35. Law 17:11- Ni damu inayofanya upatanisho- Rum. 3:23-24; 1 Yohana 1:7

36. Law 23:36-37- Sadaka ya Kinywaji: “Mtu akiona kiu”- Yohana 7:37

37. Hesabu 9:12 -Hakuna mfupa Wake uliovunjwa- Yohana 19:31-36

38. Hesabu 21:9 -Kama Nyoka juu ya mti - Kristo aliinua- Yohana 3:14-18; 12:32

39. Hesabu 24:17- Wakati huo: “Nitamwona, lakini si sasa.”- Yohana 1:14; Gal 4:4

40. Kumb 18:15 -“Kweli Huyu ni Nabii Yule”- Yohana 6:14

41. Kumb 18:15-16- “Kama mngalimwamini Musa, mngaliniamini Mimi.-” Yohana 5:45-47

42. Kumb 18:18- Aliyetumwa na Baba kusema Neno Lake- Yohana 8:28-29

43. Kumb 18:19 -Yeyote asiyesikiliza lazima abebe dhambi Yake- Matendo 3:22-23

44. Kumb 21:23 -Amelaaniwa aangikwaye juu ya mti-- Gal 3:10-13

45. Yoshua 5:14-15- Kapteni wa wokovu wetu -Ebr 2:10

46. Ruthu 4:4-10 -Kristo, Ndugu yetu, ametukomboa- Efe 1:3-7

47. 1 Sam 2:35 -Kuhani Mwaminifu -Ebr 2:17; 3:1-3, 6; 7:24-25

48. 1 Sam 2:10 -Atakuwa Mfalme aliyepakwa mafuta kwa Bwana- Mathayo 28:18; Yohana 12:15

49. 2 Sam 7:12 -Uzao wa Daudi- Mathayo 1:1

50. 2 Sam 7:13 -Ufalme Wake ni wa milele -2 Pet 1:11

51. 2 Sam 7:14a- Mwana wa Mungu- Luka 1:32; Rum 1:3-4

52. 2 Sam 7:16 -Nyumba ya Daudi ilianzishwa milele- Luka 3:31; Ufu 22:16

53. 2 Wafalme 2:11- Kupaa mbinguni kimwili kuliashiria- Luka 24:51

54. 1 Nyakati 17:11- Uzao wa Daudi- Mathayo 1:1; 9:27

55. 1 Nyakati 17:12-13-Atatawala katika kiti cha enzi cha Daudi milele- Luka 1:32-33

56. 1 Nyakati 17:13- “Nitakuwa Baba Yake, Yeye...Mwanangu.”- Ebr 1:5

57. Ayubu 9:32-33 -Mpatanishi kati ya mwanadamu na Mungu -1 Tim 2:5

58. Ayubu 19:23-27- Ufufuo ulitabiriwa- Yohana 5:24-29

59. Zaburi 2:1-3 -Uadui wa wafalme uliopangwa tangu mwanzo- Matendo 4:25-28

60. Zaburi 2:2 -Kumiliki cheo, Mpakwa Mafuta (Kristo)- Yohana 1:41; Matendo 2:36

61. Zaburi 2:6 -Tabia Yake-Utakatifu- Yohana 8:46; Ufu 3:7

62. Zaburi 2:6 -Kumiliki cheo Mfalme -Mathayo 2:2

63. Zaburi 2:7 -Alimtangaza Mwana Mpendwa- Mathayo 3:17; Warumi 1:4

64. Zaburi 2:7-8- Kusulubiwa na Kufufuka kulielezea- Matendo 13:29-33

65. Zaburi 2:8-9- Atatawala mataifa kwa fimbo ya chuma- Ufunuo 2:27; 12:5; 19:15

66. Zaburi 2:12 -Uzima huja kwa imani katika Yeye- Yohana 20:31

67. Zaburi 8:2- Vinywa vya watoto wachanga hukamilisha sifa Zake- Mathayo 21:16

68. Zaburi 8:5-6 -Kudhalilishwa na kuinuliwa Kwake- Ebr 2:5-9

69. Zaburi 9:7-10- Atahukumu ulimwengu kwa haki- Matendo 17:31

70. Zaburi 16:10- Hakutaka kuona uharibifu- Matendo 2:31; 13:35

71. Zaburi 16:9-11- Angefufuka kutoka kwa wafu- Yohana 20:9

72. Zaburi 17:15 Ufufuo ulitabiriwa- Luka 24:6

73. Zaburi 18:2-3 Pembe ya wokovu- Luka 1:69-71

74. Zaburi 22:1- Kuachwa kwa sababu ya dhambi za wengine- 2 Kor 5:21

75. Zaburi 22:1- "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?"- Mathayo 27:46

76. Zaburi 22:2 -Giza juu ya Kalvari kwa saa tatu- Mathayo 27:45

77. Zaburi 22:7- Wanapiga kelele na kutikisa kichwa- Mathayo 27:39-44

78. Zaburi 22:8- "Alimtumaini Mungu, na amwokoe"- Mathayo 27:43

79. Zaburi 22:9-10- Alizaliwa Mwokozi- Luka 2:7

80. Zaburi 22:12-13- Wanatafuta kumwuua- Yohana 19:6

81. Zaburi 22:14- Damu Yake ilimwagika walipomchoma ubavuni- Yohana 19:34

82. Zaburi 22:14-15- Aliteseka sana pale Kalvari-Mark 15:34-37

83. Zaburi 22:15 -Aliona kiu -Yohana- 19:28

84. Zaburi 22:16 -Wamtoboa mikono na miguu- Yohana 19:34-37; 20:27

85. Zaburi 22:17-18- Walimvua nguo zake mbele ya macho ya watu- Luka 23:34-35

86. Zaburi 22:18- Waligawanya mavazi Yake- Yohana 19:23-24

87. Zaburi 22:20-21- Alijikabidhi kwa Mungu- Luka 23:46

88. Zaburi 22:20-21- Nguvu za Shetani zikimchubua Mkombozi kisigino- Ebr 2:14

89. Zaburi 22:22 -Ufufuo Wake ulitangazwa- Yohana 20:17

90. Zaburi 22:27-28- Atakuwa mtawala wa mataifa- Kol 1:16

91. Zaburi 22:31- “Imekwisha”- Yohana 19:30; Ebr 10:10-12, 14, 18

92. Zaburi 23:1- “Mimi Ndimi Mchungaji Mwema”- Yohana 10:11; 1 Pet 2:25

93. Zaburi 24:3- Kuinuliwa Kwake kulitabiri- Matendo 1:11; Wafilipi 2:9

94. Zaburi 30:3 Ufufuo Wake ulitabiri- Matendo 2:32

95. Zaburi 31:5- “Mikononi Mwako naiweka roho Yangu”- Luka 23:46

96. Zaburi 31:11- Marafiki Zake walimkimbia- Marko 14:50

97. Zaburi 31:13- Wakafanya shauri la kumwua- Mathayo 27:1; Yohana 11:53

98. Zaburi 31:14-15- “Alimtumaini Mungu, sasa na amwokoe”- Mathayo 27:43

99. Zaburi 34:20- Hakuna hata mfupa Wake uliovunjika- Yohana 19:31-36

100. Zaburi 35:11- Mashahidi wa uongo walisimama dhidi Yake- Mathayo 26:59

101. Zaburi 35:19- Alichukiwa bila sababu- Yohana 15:25

102. Zaburi 38:11- Marafiki Zake walisimama mbali- Luka 23:49

103. Zaburi 38:12- Maadui walijaribu kumnasa kwa hila- Marko 14:1; Mathayo 22:15

104. Zaburi 38:12-13- alikaa kimya mbele ya washtaki Wake- Mathayo 27:12-14

105. Zaburi 38:20 -Alizunguka-zunguka akitenda mema -Matendo 10:38

106. Zaburi 40:2-5- Furaha ya ufufuo Wake ilitabiriwa- Yohana 20:20

107. Zaburi 40:6-8- Furaha Yake—mapenzi ya Baba- Yohana 4:34; Ebr 10:5-10

108. Zaburi 40:9- Alipaswa kuhubiri Haki katika Israeli- Mathayo 4:17

109. Zaburi 40:14- Kukabiliwa na maadui katika Bustani- Yohana 18:4-6

110. Zaburi 41:9- Kusalitiwa na rafiki anayemfahamu- Yohana 13:18

111. Zaburi 45:2 -Maneno ya Neema yanatoka midomoni Mwake- Yohana 1:17; Luka 4:22

112. Zaburi 45:6 -Kumiliki cheo, Mungu au Elohim- Ebr 1:8

113. Zaburi 45:7- Upako maalum wa Roho Mtakatifu- Math 3:16; Ebr 1:9

114. Zaburi 45:7-8- Yeye Anayeitwa Kristo (Masihi au Mpakwa Mafuta)- Luka 2:11

115. Zaburi 45:17- Jina Lake likumbukwe milele- Efe 1:20-21; Ebr 1:8

116. Zaburi 55:12-14- Alisalitiwa na rafiki, si adui- Yohana 13:18

117. Zaburi 55:15- Kifo kisichotubu cha Msaliti- Math 27:3-5; Matendo 1:16-19

118. Zaburi 68:18- Kuwapa wanadamu zawadi- Waefeso 4:7-16

119. Zaburi 68:18 -Alipaa Mbinguni- Luka 24:51

120. Zaburi 69:4- Alichukiwa bila sababu- Yohana 15:25

121. Zaburi 69:8 -Mgeni kwa ndugu Zake- Yohana 1:11; 7:5

122. Zaburi 69:9- Mwenye Bidii kwa Nyumba ya Bwana- Yohana 2:17

123. Zaburi 69:14-20- Uchungu wa Masihi wa roho kabla ya kusulubiwa- Mathayo 26:36-45

124. Zaburi 69:20- “Nafsi Yangu ina huzuni nyingi”- Mathayo 26:38

125. Zaburi 69:21 -Aliyepewa siki alipokuwa na kiu- Mathayo 27:34

126. Zaburi 69:26- Mwokozi Alitolewea kafara na kupigwa na Mungu -Yohana 17:4; 18:11

127. Zaburi 72:10-11- Watu wakuu wangemtembelea- Mathayo 2:1-11

128. Zaburi 72:16 -Chembe ya ngano kuanguka ardhini- Yohana 12:24-25

129. Zaburi 72:17- Imani katika Jina Lake itazaa watoto- Yohana 1:12-13

130. Zaburi 72:17- Mataifa yote yatabarikiwa Naye- Gal 3:8

131. Zaburi 72:17- Mataifa yote yatamwita mbarikiwa- Yohana 12:13; Ufunuo 5:8-12

132. Zaburi 78:12- Angefundisha kwa mifano- Mathayo 13:34-35

133. Zaburi 78:2b- Kutangaza Hekima ya Mungu kwa mamlaka- Mathayo 7:29

134. Zaburi 80:17- Mkono wa kuume wa Mtu wa Mungu- Marko 14:61-62

135. Zaburi 88 -Mateso na Laana ya Kalvari- Mathayo 27:26-50

136. Zaburi 88:8 -Walisimama mbali na kumtazama- Luka 23:49

137. Zaburi 89:27- Mzaliwa wa kwanza- Kol 1:15-18

138. Zaburi 89:27 -Imanueli ni mkuu kuliko wafalme wa kidunia- Luka 1:32-33

139. Zaburi 89:35-37- Uzao wa Daudi, kiti cha enzi, ufalme wadumu milele- Luka 1:32-33

140. Zaburi 89:36-37 -Tabia Yake-Uaminifu- Ufu 1:5; 19:11

141. Zaburi 90:2- Yeye ni wa milele- (Mika 5:2) Yohana 1:1

142. Zaburi 91:11-12 -Alitambuliwa kama Masihi,  Kristo atajaribiwa- Luka 4:10-11

143. Zaburi 97:9 -Kuinuliwa Kwake kulitabiri- Matendo 1:11; Efe 1:20

144. Zaburi 100:5 -Tabia Yake-Wema Mathayo- 19:16-17

145. Zaburi 102:1-11- Mateso na Lawama za Kalvari- Yohana 19:16-30

146. Zaburi 102:25-27- Masihi Ndiye Mwana Aliyekuwepo Zamani- Waebrania 1:10-12

147. Zaburi 109:25 -Alidhihakiwa- Mathayo 27:39

148. Zaburi 110:1- Mwana wa Daudi- Mathayo 22:42-43

149. Zaburi 110:1 -Apaa hadi mkono wa kuume wa Baba- Marko 16:19

150. Zaburi 110:1 -Mwana wa Daudi aitwaye Bwana- Mathayo 22:44-45

151. Zaburi 110:4- Kuhani kwa utaratibu wa Melkizedeki- Waebrania 6:20

152. Zaburi 112:4 -Tabia Yake-Mwenye Huruma, Neema, et al- Mathayo 9:36

153. Zaburi 118:17-18- Ufufuo wa Masihi wahakikishwa -Luka 24:5-7; 1 Kor 15:20

154. Zaburi 118:22-23- Jiwe lililokataliwa ni Msingi wa  pembeni mwa jengo -Mathayo 21:42-43

155. Zaburi 118:26a- Aliyebarikiwa awasilishwa kwa Israeli- Mathayo 21:9

156. Zaburi 118:26b -Atakuja Hekaluni, likiwa limesimama- Mathayo 21:12-15

157. Zaburi 132:11- Uzao wa Daudi (tunda la Mwili Wake)- Luka 1:32; Matendo 2:30

158. Zaburi 129:3- Alipigwa mijeledi -Mathayo 27:26

159. Zaburi 138:1-6 -Ukuu wa Uzao wa Daudi wawashangaza wafalme- Mathayo 2:2-6

160. Zaburi 147:3-6- Huduma ya Kristo duniani ilielezewa- Luka 4:18

161. Mithali 1:23 -Atatuma Roho wa Mungu -Yohana 16:7

162. Mithali 8:23- Aliyechaguliwa tangu milele -Ufunuo 13:8; 1 Pet 1:19-20

163. Wimbo 5:16- Yule bora kabisa- Yohana 1:17

164. Isaya 2:3 -Atawafundisha mataifa yote- Yohana 4:25

165. Isa 2:4 -Atahukumu miongoni mwa mataifa -Yohana 5:22

166. Isa 6:1- Isaya alipoona utukufu Wake -Yohana 12:40-41

167. Isa 6:8 -Aliyetumwa na Mungu -Yohana 12:38-45

168. Isa 6:9-10 -Mifano Yake huanguka kwenye masikio ya viziwi- Mathayo 13:13-15

169. Isa 6:9-12- Watakuwa Vipofu na viziwi kwa Maneno Yake Kristo-Matendo 28:23-29

170. Isa 7:14- Kuzaliwa na bikira -Luka 1:35

171. Isa 7:14- Atakuwa Imanueli-Mungu pamoja nasi- Mathayo 1:18-23; 1 Tim 3:16

172. Isa 8:8 -Anaitwa Emmanueli -Mathayo 28:20

173. Isa 8:14- Jiwe la kujikwaa, Mwamba wa kukwaza -1 Pet 2:8

174. Isa 9:1-2 -Huduma Yake itaanza Galilaya- Mathayo 4:12-17

175. Isa 9:6 -Mtoto aliyezaliwa- Mwenye Uungu na Ubinadamu- Luka 1:31

176. Isa 9:6 -Mwana aliyepewa-Uungu Luka 1:32; Yohana 1:14; 1 Tim 3:16

177. Isa 9:6- Alitangazwa kuwa Mwana wa Mungu Mwenye nguvu- Rum 1:3-4

178. Isa 9:6- Mtu wa Ajabu, Peleh- Luka 4:22

179. Isa 9:6- Mshauri, Yaatz -Mathayo 13:54

180. Isa 9:6- Mungu Mwenye Nguvu, El Gibor- 1 Kor 1:24; Tito 2:3

181. Isa 9:6- Baba wa Milele, Avi Adth -Yohana 8:58; 10:30

182. Isa 9:6- Mfalme wa Amani, Sar Shalom- Yohana 16:33

183. Isa 9:7- Ataanzisha ufalme wa milele -Luka 1:32-33

184. Isa 9:7- Tabia Yake-Mwaminifu -Yohana 5:30

185. Isa 9:7- Hakuna mwisho wa Serikali Yake, Kiti cha Enzi, na Amani- Luka 1:32-33

186. Isa 11:1- Kuitwa Mnazareti-Tawi, Nezer -Mathayo 2:23

187. Isa 11:1- Fimbo kutoka kwa Yese-Mwana wa Yese -Luka 3:23-32

188. Isa 11:2- Aliyepakwa Mafuta kwa Roho- Mathayo 3:16-17; Matendo 10:38

189. Isa 11:2- Tabia Yake-Hekima, Maarifa, na mengine- Kol 2:3

190. Isa 11:3- Angejua mawazo yao- Luka 6:8; Yohana 2:25

191. Isa 11:4- atahukumu kwa haki- Matendo 17:31

192. Isa 11:4 -Atahukumu kwa upanga wa kinywa Chake- Ufu 2:16; 19:11, 15

193. Isa 11:5- Tabia: Mwenye Haki na Mwaminifu- Ufunuo 19:11

194. Isa 11:10- Mataifa Wanamtafuta -Yohana 12:18-21

195. Isa 12:2 -Ataitwa Yesu-Yeshua -Mathayo 1:21

196. Isa 22:22- Yule aliyepewa mamlaka yote ya kutawala -Ufunuo 3:7

197. Isa 25:8- Ufufuo Ulitabiriwa- 1 Kor 15:54

198. Isa 26:19- Nguvu Yake ya Ufufuo ilitabiriwa -Mathayo 27:50-54

199. Isa 28:16- Masihi Ndiye jiwe la pembeni la thamani -Matendo 4:11-12

200. Isa 28:16- Msingi Ulio imara 1 Kor 3:11;- Mathayo 16:18

201. Isaya 29:13- Alionyesha utii wa kinafiki kwa Neno Lake- Mathayo 15:7-9

202. Isaya 29:14- Wenye hekima huaibishwa na Neno- 1 Kor 1:18-31

203. Isaya 32:2- Kimbilio-Atakuwa mahali pa kujificha- Mathayo 23:37

204. Isaya 35:4- Atakuja na kuwaokoa- Mathayo 1:21

205. Isaya 35:5-6- Atakuwa na huduma ya miujiza- Mathayo 11:2-6

206. Isa 40:3-4- Iliyotanguliwa na mtangulizi- Yohana 1:23

207. Isa 40:9- “Tazameni Mungu wenu” -Yohana 1:36; 19:14

208. Isa 40:10- Atakuja kutuza- Ufunuo 22:12

209. Isa 40:11- Mchungaji-mtoaji wa maisha Mwenye huruma-Yohana 10:10-18

210. Isa 42:1-4- Mtumishi-kama mkombozi mwaminifu na mvumilivu- Mathayo 12:18-21

211. Isa 42:2 -Mpole na mnyenyekevu- Mathayo 11:28-30

212. Isa 42:3- Anawaletea tumaini wasio na tumaini- Yohana 4

213. Isa 42:4- Mataifa yatasubiri mafundisho Yake- Yohana 12:20-26

214. Isa 42:6 -Nuru (wokovu) wa Mataifa- Luka 2:32

215. Isa 42:1-6- Huruma Yake ya duniani kote- Mathayo 28:19-20

216. Isa 42:7- Macho ya vipofu yalifunguliwa -Yohana 9:25-38

217. Isa 43:11 -Yeye Ndiye Mwokozi pekee- Matendo 4:12

218. Isa 44:3- Atatuma Roho wa Mungu- Yohana 16:7-13

219. Isa 45:21-25- Yeye ni Bwana na Mwokozi -Wafilipi 3:20; Tito 2:13

220. Isa 45:23- Yeye atakuwa Mwamuzi- Yohana 5:22; Warumi 14:11

221. Isa 46:9-10- Anatangaza mambo ambayo hayajafanyika -Yohana 13:19

222. Isa 48:12- Wa Kwanza na Wa Mwisho- Yohana 1:30; Ufunuo 1:8, 17

223. Isa 48:16-17- Alikuja kama Mwalimu -Yohana 3:2

224. Isa 49:1- Aliitwa kutoka tumboni-Ubinadamu Wake -Mathayo 1:18

225. Isa 49:5- Mtumishi kutoka tumboni- Luka 1:31; Wafilipi 2:7

226. Isa 49:6- Atairejesha Israeli- Matendo 3:19-21; 15:16-17

227. Isa 49:6 -Yeye ni Wokovu kwa Israeli- Luka 2:29-32

228. Isa 49:6- Yeye ni Nuru ya Mataifa -Yohana 8:12; Matendo 13:47

229. Isa 49:6- Yeye ni Wokovu hadi miisho ya dunia- Matendo 15:7-18

230. Isa 49:7 -Atadharauliwa na Taifa -Yohana 1:11; 8:48-49; 19:14-15

231. Isa 50:3- Mbingu zimefunikwa na giza kwaajili ya aibu Yake- Luka 23:44-45

232. Isa 50:4 -Yeye ni mshauri Mwenye hekima na maarifa kwa waliochoka -Mathayo 7:29; 11:28-29

233. Isa 50:5 -Mtumishi aliyefungwa kwa hiari na kwa utii -Mathayo 26:39

234. Isa 50:6a -“Niliwapa mgongo Wangu wale walionipiga” -Mathayo 27:26

235. Isa 50:6b -Alipigwa mashavuni- Mathayo 26:67

236. Isa 50:6c -Alitemewa mate- Mathayo 27:30

237. Isa 52:7- Alitangaza habari njema juu ya milima- Mathayo 5:12; 15:29; 28:16

238. Isa 52:13- Mtumishi aliyetukuzwa -Matendo 1:8-11; Waefeso 1:19-22; Wafilipi 2:5-9

239. Isa 52:14- Mtumishi aliyetukana kwa njia ya kushangaza -Luka 18:31-34; Mathayo 26:67-68

240. Isa 52:15- Mataifa yalishtushwa na ujumbe wa Mtumishi- Luka 18:31-34; Mathayo 26:67-68

241. Isa 52:15- Damu Yake iliyomwagika yanyunyizia mataifa- Ebr 9:13-14; Ufunuo 1:5

242. Isa 53:1 -Watu  Wake hawakumwamini -Yohana 12:37-38

243. Isa 53:2- Ataonekana kama mtu wa kawaida -Wafilipi 2:6-8

244. Isa 53:3a- Alidharauliwa- Luka 4:28-29

245. Isa 53:3b- Alikataliwa -Mathayo 27:21-23

246. Isa 53:3c -Huzuni kubwa na sikitiko- Mathayo 26:37-38; Luka 19:41; Ebr 4:15

247. Isa 53:3d- Watu hujificha wasihusiane Naye- Marko 14:50-52

248. Isa 53:4a -Angepata uponyaji- Mathayo 8:16-17

249. Isa 53:4b -Alidhaniwa amelaaniwa na Mungu- Mathayo 26:66; 27:41-43

250. Isa 53:5a -Amebeba adhabu kwa maovu ya wanadamu- 2 Kor 5:21; Ebr 2:9

251. Isa 53:5b -Sadaka Yake hutoa amani kati ya mwanadamu na Mungu- Kol 1:20

252. Isa 53:5c -Sadaka Yake ingemponya mwanadamu dhambi- 1 Pet 2:24

253. Isa 53:6a -Angekuwa mchukua dhambi kwa wanadamu wote- 1 Yohana 2:2; 4:10

254. Isa 53:6b -Ni Mapenzi ya Mungu kwamba achukue dhambi kwa ajili ya wanadamu wote- Gal 1:4

255. Isa 53:7a- Mtumishi aliyeonewa na kuteswa- Mathayo 27:27-31

256. Isa 53:7b- Alikaa kimya mbele ya washtaki Wake- Mathayo 27:12-14

257. Isa 53:7c- Mwana-Kondoo wa dhabihu -Yohana 1:29; 1 Pet 1:18-19

258. Isa 53:8a -Alifungwa na kuteswa- Mathayo 26:47-27:31

259. Isa 53:8b -Angehukumiwa- Yohana 18:13-22

260. Isa 53:8c -Aliuawa- Mathayo 27:35

261. Isa 53:8d -Alikufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu- 1 Yohana 2:2

262. Isa 53:9a -Alizikwa katika kaburi la tajiri- Mathayo 27:57

263. Isa 53:9b Asiyekuwa na hatia na hakufanya vurugu- Luka 23:41; Yohana 18:38

264. Isa 53:9c- Hakuna udanganyifu au hila kinywani Mwake- 1 Pet 2:22

265. Isa 53:10a- Ni Mapenzi ya Mungu kwamba afe kwa ajili ya wanadamu- Yohana 18:11

266. Isa 53:10b- Ni Sadaka kwa ajili ya dhambi- Mathayo 20:28; Gal 3:13

267. Isa 53:10c -Atafufuliwa na kuishi milele- Rum 6:9

268. Isa 53:10d -Angefanikiwa -Yohana 17:1-5

269. Isa 53:11a- Mungu aliridhika kikamilifu na mateso Yake -Yohana 12:27

270. Isa 53:11b -Mtumishi wa Mungu angemhesabia haki mwanadamu -Rum 5:8-9, 18-19

271. Isa 53:11c- Mbeba dhambi kwa ajili ya wanadamu wote- Ebr 9:28

272. Isa 53:12a- Alimeinuliwa na Mungu kwa sababu ya dhabihu Yake- Mathayo 28:18

273. Isa 53:12b- Angetoa maisha Yake ili kuwaokoa wanadamu- Luka 23:46

274. Isa 53:12c- Alihesabiwa pamoja na wakosaji -Marko 15:27-28

275. Isa 53:12d- Mbeba dhambi za wanadamu wote -1 Pet 2:24

276. Isa 53:12e -Mwombezi kwa Mungu kwa niaba ya wanadamu- Luka 23:34; Warumi 8:34

277. Isa 55:3 -Angefufuliwa na Mungu- Matendo 13:34

278. Isa 55:4a- Shahidi -Yohana 18:37

279. Isa 55:4b -Yeye ni kiongozi na Amiri Jeshi- Ebr 2:10

280. Isa 55:5 -Mungu angemtukuza- Matendo 3:13

281. Isa 59:16a- Mwombezi kwaajili ya wanadamu kwa Mungu- Mathayo 10:32

282. Isa 59:16b- Angekuja kutoa wokovu -Yohana 6:40

283. Isa 59:20- Angekuja Sayuni kama Mkombozi wao- Luka 2:38

284. Isa 60:1-3- Angeonyesha nuru kwa Mataifa -Matendo 26:23

285. Isa 61:1a- Roho wa Mungu juu Yake- Mathayo 3:16-17

286. Isa 61:1b- Masihi angehubiri habari njema -Luka 4:16-21

287. Isa 61:1c -Angetoa uhuru kutoka kwa utumwa wa dhambi-Yohana 8:31-36

288. Isa 61:1-2a- Angetangaza kipindi cha neema- Gal 4:4-5

289. Yer 23:5-6 -Uzao wa Daudi -Luka 3:23-31

290. Yer 23:5-6 -Masihi angekuwa Mungu na Mwanadamu -Yohana 13:13; 1 Tim 3:16

291. Yer 31:22 -Alizaliwa na bikira -Math 1:18-20

292. Yer 31:31 -Masihi angeweka Agano Jipya- Math 26:28

293. Yer 33:14-15- Uzao wa Daudi- Luka 3:23-31

294. Ezek 34:23-24- Uzao wa Daudi -Math 1:1

295. Ezek 37:24-25- Uzao wa Daudi -Luka 1:31-33

296. Dan 2:44-45- Jiwe litakalovunja falme -Math 21:44

297. Dan 7:13-14a -Angepaa mbinguni -Matendo 1:9-11

298. Dan 7:13-14b- Yeye Aliyeinuliwa sana- Efe 1:20-22

299. Dan 7:13-14c -Utawala wake ungekuwa wa milele- Luka 1:31-33

300. Dan 9:24a -Atakomesha dhambi- Gal 1:3-5

301. Dan 9:24a- Atafanya upatanisho kwa ajili ya uovu- Rum 5:10; 2 Kor 5:18-21

302. Dan 9:24b- Ni mtakatifu- Luka 1:35

303. Dan 9:25- Tangazo Lake- Yohana 12:12-13

304. Dan 9:26a- Kukatiliwa mbali- Mathayo 16:21; 21:38-39

305. Dan 9:26b- Kufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu- Ebr 2:9

306. Dan 9:26c- Aliuawa kabla ya kuharibiwa kwa hekalu- Math 27:50-51

307. Dan 10:5-6- Masihi katika hali ya utukufu- Ufu 1:13-16

308. Hos 11:1 -Angeitwa kutoka Misri -Math 2:15

309. Hos 13:14 -Angeshinda kifo -1 Kor 15:55-57

310. Yoeli 2:32- Atatoa wokovu kwa wanadamu wote- Rum 10:9-13

311. Yona 1:17- Kifo na ufufuo wa Kristo- Math 12:40; 16:4

312. Mika 5:2a -Alizaliwa Bethlehemu- Mathayo 2:1-6

313. Mika 5:2b -Mtawala wa Israeli- Luka 1:33

314. Mika 5:2c- Yeye ni wa milele mbele na nyuma- Yohana 8:58

315. Hag 2:6-9- Angetembelea Hekalu la pili- Luka 2:27-32

316. Hag 2:23- Uzao wa Zerubabeli -Luka 2:27-32

317. Zek 3:8 -Mtumishi wa Mungu- Yohana 17:4

318. Zek 6:12-13- Kuhani na Mfalme- Ebr 8:1

319. Zek 9:9a -Alikaribishwa kwa furaha Yerusalemu -Mathayo 21:8-10

320. Zek 9:9b -Alionwa kama Mfalme -Yohana 12:12-13

321. Zek 9:9c -Ni Masihi- Yohana wa haki 5:30

322. Zek 9:9d -Masihi angeleta wokovu- Luka 19:10

323. Zek 9:9e -Masihi angekuwa mnyenyekevu- Mathayo 11:29

324. Zek 9:9f -Aliwasilishwa Yerusalemu akiwa amepanda punda -Mathayo 21:6-9

325. Zek 10:4 -Jiwe la pembeni- Efe 2:20

326. Zek 11:4-6a -Wakati wa kuja Kwake, Israeli itakuwa na viongozi wasiofaa- Mathayo 23:1-4

327. Zek 11:4-6b- Kukataliwa kunamfanya Mungu aondoe ulinzi Wake- Luka 19:41 -44

328. Zek 11:4-6c -Alikataliwa, na mfalme mwingine akawekwa mbadala Wake - Yohana 19:13-15

329. Zek 11:7- Huduma kwa "maskini," masalio waaminio- Mathayo 9:35-36

330. Zek 11:8a- Kutoamini kunamlazimisha Masihi kuwakataa- Mathayo 23:33

331. Zek 11:8b- Anadharauliwa -Mathayo 27:20

332. Zek 11:9 -Anaacha kuwahudumia wale waliomkataa- Mathayo 13:10-11

333. Zek 11:10-11a- Kukataliwa kunamfanya Mungu aondoe ulinzi- Luka 19:41-44

334. Zek 11:10-11b- Masihi angekuwa Mungu- Yohana 14:7

335. Zek 11:12-13a -Alisalitiwa kwa vipande 30 vya fedha -Mathayo 26:14-15

336. Zek 11:12-13b- Alikataliwa- Mathayo 26:14-15

337. Zek 11:12-13c- Vipande 30 vya fedha vilivyotupwa katika nyumba ya Bwana- Mathayo 27:3-5

338. Zek 11:12-13d- Masihi Ni Mungu- Yohana 12:45

339. Zek 12:10a- Mwili wa Masihi ungechomwa mkuki -Yohana 19:34-37

340. Zek 12:10b -Masihi angekuwa Mungu na mwanadamu- Yohana 10:30

341. Zek 12:10c- Masihi angekataliwa -Yohana 1:11

342. Zek 13:7a -Mpenzi wa Mungu Angekufa kwa ajili ya wanadamu -Yohana 18:11

343. Zek 13:7b -Kifo cha kikatili Alama -Yohana 14:27

344. Zek 13:7c- Mungu na mwanadamu- Yohana 14:9

345. Zek 13:7d- Israeli walitawanyika kutokana na kumkataa- Mathayo 26:31-56

346. Zek 14:4 -Angerudi kwenye Mlima wa Mizeituni -Matendo 1:11-12

347. Mal 3:1a -Mjumbe wa kuandaa njia kwa ajili ya Masihi -Marko 1:1-8

348. Mal 3:1b -Kuonekana ghafla hekaluni- Marko 11:15-16

349. Mal 3:1c- Mjumbe wa Agano Jipya- Luka 4:43

350. Mal 4:5- Mtangulizi katika roho ya Eliya -Mathayo 3:1-3; 11:10-14; 17:11-13

351. Mal 4:6 -Mtangulizi angewageuza wengi kwenye haki- Luka 1:16-17

(Joint Base Elmendorf / Richardson)

Muhtasari wa Kitabu NGAZI YA KUFIKA MBINGUNI-**Ninawezaje Kuja Kwa MWENYEZI MUNGU?**

*Sehemu ya Kwanza*

Asili na ufunuo wa Mungu kwa wanadamu, vyote kwa pamoja hushuhudia upendo wa Mungu. Ni uvunjaji (uasi) wa Sheria ya Mungu, Sheria ya upendo, ndio imeleta misiba na kifo. Lakini hata katikati ya mateso yanayotokana na dhambi, upendo wa Mungu unafunuliwa. “Mungu ni upendo” imeandikwa juu ya kila chipukizi, juu ya kila unyasi unaochipuka.

Masihi alikuja kuishi miongoni mwa wanadamu ili kudhihirisha upendo wa Mungu usio na kikomo. Upendo, rehema, na huruma zilikuwa zimefunuliwa katika kila tendo la maisha Yake; Moyo Wake ulikwenda kwa huruma nyororo, mapenzi mwanana, na kujali, kwa watoto wa wanadamu. Alichukua asili ya mwanadamu, ili Aweze kufikia matakwa ya mwanadamu. Maskini na wanyenyekevu zaidi hawakuogopa kumkaribia Yeye. Hiyo ndiyo tabia ya Kristo kama inavyofunuliwa katika maisha Yake. Hii ndiyo tabia ya Mungu.

Ilikuwa ni kwa ajili ya kutukomboa ndiyo maana Yesu aliishi, aliteseka, na kufa. Alifanyika “Mtu wa Huzuni,” ili sisi tupate kufanywa washirika wa furaha ya milele. Lakini dhabihu hii kuu haikutolewa ili kuunda katika Moyo wa Baba upendo kwa mwanadamu, sio kumfanya awe tayari kutuokoa. Hapana, hapana! “Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee.” Yohana 3:16. Baba anatupenda, sio kwa sababu ya upatanisho mkuu, bali Yeye Alitoa upatanisho kwa sababu anatupenda. Hakuna mwingine ila Mwana wa Mungu Ndiye Ambaye angeweza kutimiza ukombozi wetu.

Hii inaweka thamani iliyoje kwa mwanadamu! Kupitia uasi, wana wa wanadamu wanakuwa raia wa Shetani. Kupitia imani katika dhabihu ya upatanisho ya Kristo, wana wa Adamu wanaweza kuwa wana wa Mungu. Upendo usio na kifani wa Mungu kwa ulimwengu ambao haukumpenda! Mawazo yana nguvu ya kutiisha juu ya nafsi na huleta akili katika utumwa wa mapenzi ya Mungu.

Mwanadamu hapo awali alijaliwa uwezo bora na akili iliyo na utimamu mzuri. Alikuwa mkamilifu katika nafsi yake, na mapatano na Mungu. Mawazo yake yalikuwa safi, malengo yake yalikuwa matakatifu. Lakini kwa kutokutii, nguvu zake zilipotoshwa, na ubinafsi ukachukua nafasi ya upendo. Asili yake ilidhoofika sana kupitia dhambi ambayo haikuwezekana kwake, kwa nguvu zake mwenyewe, kupinga nguvu za uovu.

Haiwezekani sisi, naam, sisi wenyewe, kuepuka shimo la dhambi ambalo tumezama ndani yake. Mioyo yetu ni miovu, na hatuwezi kujibadilisha. Lazima kuwe na nguvu inayofanya kazi kutoka ndani, maisha mapya kutoka juu, kabla ya sisi wanadamu kubadilishwa kutoka katika dhambi hadi utakatifu. Nguvu hiyo ni Kristo. Neema Yake pekee ndiyo inayoweza kuhuisha uwezo usio na uhai wa nafsi, na kutuvuta kwa Mungu, kwa utakatifu. Kwa wote, kuna jibu moja tu, Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yohana 1:29. Hebu na tuikubali njia hii iliyotolewa kwa ajili yetu ili tuweze kugeuzwa na kufanana Naye, na kurejeshwa katika ushirika na malaika wanaohudumia, kwa maelewano na ushirika na Baba na Mwana.

Mtu atakuwaje mwenye haki mbele za Mungu? Mwenye dhambi atafanywaje kuwa mwadilifu? Ni kwa njia ya Kristo pekee tunaweza kuletwa katika mapatano na Mungu, kwa utakatifu; lakini tunawezaje kumwendea Kristo?

Toba ni pamoja na huzuni kwa ajili ya dhambi na kuiacha. Hatutaacha dhambi mpaka tuone ubaya wake; mpaka tuiache kwa moyo, hakutakuwa na mabadiliko ya kweli katika maisha. Lakini moyo

unapokubali kuongozwa na Roho wa Mungu, dhamiri itahuishwa, na mwenye dhambi atatambua jambo fulani la kina, na utakatifu wa Sheria takatifu ya Mungu, na msingi Wa serikali Yake mbinguni na duniani. Kisha usadikisho hushika akili na moyo.

Ombi la Daudi, baada ya anguko lake, linaonyesha asili ya huzuni ya kweli kwa ajili ya dhambi. Toba yake ilikuwa ya dhati na ya kina. Hakukuwa na jitihada za kutuliza hatia yake; hakuwa na hamu ya kutoroka hukumu inayomtishia ila aliongozwa katika maombi yake. Daudi aliona ukubwa wa kosa lake; aliona unajisi wa nafsi yake; yeye aliichukia dhambi yake. Haikuwa kwa ajili ya msamaha tu kwamba aliomba, lakini kwa ajili ya usafi wa moyo. Alitamani furaha ya utakatifu, kurejeshwa katika maelewano na ushirika na Mungu.Toba kama hii haiwezi kufikiwa na uwezo wetu wenyewe na kuikamilisha; bali hupatikana tu kutoka Kristo.

Kristo Yuko tayari kutuweka sisi huru kutokana na dhambi, lakini halazimishi nia hiyo. Tukikataa, Je, Yeye anaweza kufanya nini zaidi? Jifunze Neno la Mungu kwa maombi. Unapoona ukubwa wa dhambi maishani mwako, kama unavyojiona jinsi ulivyo, usikate tamaa kwa kupoteza matumaini. Ni wenye dhambi ndio ambao Kristo alikuja kuwaokoa. Shetani anapokuja kukuambia kuwa wewe ni mwenye dhambi mkuu, wewe mtazame Mkombozi wako na uongee juu ya wema Wake. Ikiri dhambi yako, lakini mwambie adui kwamba “Kristo alikuja ulimwenguni kuwaokoa wenye dhambi” ili mimi nipate kuokolewa (1 Timotheo 1:15).

“Afichaye dhambi zake hatafanikiwa, bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema.” Mithali 28:13. Masharti ya kupata rehema ya Mungu ni rahisi na ya haki na busara. Ungameni dhambi zenu kwa Mungu, Ambaye peke Yake Ndiye anayeweza kuwasamehe, na msameheane makosa yenu ninyi kwa ninyi. Wale ambao hawajanyenyekesha nafsi zao mbele za Mungu, kwa kukiri hatia yao, bado hawajatimiza hatua ya kwanza ya kukubalika, kwani sharti tuwe tayari kuinyenyekesha mioyo yetu na kufuata masharti ya Sheria ya Neno la Kweli. Kukiri ambako kunamiminiwa kwa roho ya ndani

hupata njia yake kwa Mungu wa huruma Asiye na kikomo. Kuungama kwa kweli siku zote huwa na tabia maalum, na hukubali dhambi fulani. Maungamo yote yanapaswa kuwa ya uhakika na ya kulenga jambo mahususi. Imeandikwa, "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." 1John 1:9.

Ahadi ya Mungu ni, "Mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa mioyo yenu yote." Yeremia 29:13. Moyo wote sharti utolewe, au mabadiliko hayawezi kamwe kufanywa ndani yetu ambayo kwayo tunapaswa kurejeshwa kwa mfano Wake Bwana.

Vita dhidi ya nafsi ni vita kubwa zaidi kuwahi kupiganwa. Kujitolea kwa nafsi, kusalimisha Mapenzi yetu yote kwa Mungu, kunahitaji mapambano; lakini nafsi inapaswa kunyenyekea kwa Mungu kabla ya kufanywa upya katika utakatifu. Katika kujitoa kwa Mungu, ni lazima kuacha yote ambayo yangetutenganisha Naye. Kuna wale wanaodai kumtumikia Mungu huku wakitegemea juhudi zao wenyewe kutii Sheria Yake, ili kuunda tabia sahihi na kupata wokovu. Mioyo yao haiguswi na hisia yoyote ya kina ya upendo wa Kristo, lakini wanatafuta kutekeleza majukumu ya maisha ya Kikristo kama vile ambavyo Mungu anataka kutoka kwao ili kuipata mbingu. Dini kama hiyo haina thamani.

Kristo akikaa ndani ya moyo, roho itajawa na upendo Wake, na furaha ya kuungana Naye, kwamba roho itashikamana Naye; na katika kumfikiria Yeye, nafsi itasahauliwa. Upendo kwa Mwenyezi Mungu utakuwa chemchemi ya kila wazo na tendo. Mambo hayo hayalengi viwango vya chini kabisa, bali hulenga kupatana kikamilifu na Mapenzi ya Mkombozi wao.

Je, unahisi kwamba ni dhabihu kubwa sana kwako kutoa yote kwa Kristo? Jiulize swali, "Ni nini Kristo ametoa kwa ajili yangu?" Mwana wa Mungu alitoa maisha yake yote, kwa upendo na akapitia mateso kwa ajili ya ukombozi wetu. Je, sisi, tusiostahili, ambao ni walengwa wa upendo mkuu hivyo, tutazuia mioyo yetu Kwake? Je, Tunatoa nini

zaidi wakati tunatoa yote? Ni Moyo uliochafuliwa na dhambi tu, ndiyo tunatoa na hakuna lingine la thamani tunalolitoa kwa Mungu, tunautoa moyo huu, ili Yesu ausafishe, ausafishe kwa damu Yake Mwenyewe, na kutuokoa kwa upendo Wake usio na kifani. Na ajabu ni kwamba, bado watu wanafikiri ni vigumu kuacha yote! (na kumbe kile tunachokiacha ni moyo mchafu tu). Mungu hataki tutoe chochote ambacho ni cha manufaa kwetu ili tubaki salama. Katika yote anayofanya, Yeye ana maslahi ya watoto Wake katika mtazamo Wake.

Wengi wanauliza, “Nifanyeje ili kujisalimisha kikamilifu kwa Mungu?” Unatamani kujitoa Kwake, lakini u dhaifu katika uwezo wa kimaadili, kisha una utumwa wa mashaka, na unatawaliwa na tabia za maisha ya dhambi. Ahadi na maazimio yako ni kama kamba za mchanga. Huwezi kudhibiti mawazo yako, misukumo yako, na mapenzi yako. Ujuzi ulio nao kuhusu ahadi zako zilizovunjwa na ahadi ulizopoteza hudhoofisha kujiamini kwako katika unyofu wako mwenyewe, na kukufanya uhisi kwamba Mungu hawezi kukukubali; lakini huna haja kukata tamaa.

Unachohitaji kuelewa ni nguvu ya kweli ya uthubutu (uchaguzi). Hii ndiyo nguvu inayotawala katika asili ya mtu, nguvu ya uamuzi, au ya kuchagua. Kila kitu kinategemea hatua sahihi ya uthubutu. Nguvu ya uhuru wa kuchagua ambao Mungu amewapa wanadamu; ni juu ya hii unapaswa kuifanyia mazoezi. Huwezi kubadilisha moyo wako, na huwezi kujibadili wewe mwenyewe, kwahiyo mpe Mungu mapenzi (matamanio) ya moyo wako; lakini unaweza kuchagua kumtumikia. Unaweza kumpa mapenzi yako; Naye Atafanya kazi ndani yako, kunia na kutenda sawasawa na mapenzi Yakemema. Kwa hivyo asili yako yote itaweza kuletwa chini ya udhibiti wa Roho wa Kristo; mapenzi yako yataelekezwa Kwake, mawazo yako yatakuwa sawa na Yeye.

Matamanio ya kuwa na wema na utakatifu ni sawa kadiri yanavyokwenda; lakini ukiishia hapa, hautafaidika kwa chochote. Wengi watapotea huku wakitumaini na kutamani kuwa Wakristo. Hawafikii hatua ya kuweka mapenzi yao kwa Mungu. Hawachagui sasa kuwa Wakristo.

Kupitia mazoezi sahihi ya uthubutu, mabadiliko yote yanaweza kufanywa katika maisha yako. Utakuwa na nguvu kutoka juu ili kukuweka imara, na hivyo kupitia kuendelea kujitoa daima kwa Mungu utawezeshwa kuishi maisha mapya, hata maisha ya imani.

Kwa vile dhamiri yako imehuishwa na Roho Mtakatifu, umeona kitu juu ya uovu/ubaya wa dhambi, na nguvu zake, hatia yake, na majanga yake; na sasa unaitazama dhambi kwa chuki. Ni amani ndiyo unayohitaji. Umeungama dhambi zako, na kuziweka mbali na moyo wako. Umeamua kujitoa kwa Mungu. Sasa nenda Kwake, na umwombe kwamba akuoshe dhambi zako na kukupa moyo mpya.

Basi amini kwamba Yeye Anafanya hivi kwa sababu ameahidi hivyo. Zawadi ambayo Mungu anatuahidi, ni sharti tuamini kwamba tunaipokea, na kwamba ni zetu. Wewe ni mwenye dhambi. Huwezi kulipia dhambi zako zilizopita; huwezi kuubadili moyo wako na kujifanya kuwa mtakatifu. Lakini Mungu anaahidi kufanya haya yote kwa ajili yako kupitia Kristo. Wewe amini tu ahadi hiyo. Tubu dhambi zako na kujitoa kwa Mungu. Utapenda kumtumikia. Vile vile unapofanya hivi, hakika Mungu atatimiza Neno Lake kwako. Ikiwa unaamini katika ahadi hiyo, Mungu anaitoa kwako kweli (kiuhalisia). Usisubiri mpaka uhisi kuwa umefanywa mzima, lakini sema, “Naamini; ni hivyo, si kwa sababu ninaihisi, bali kwa sababu Mungu “Aliahidi.”

## *Sehemu ya Pili*

### Je, ninawezaje Kubaki Mkweli kwa Kristo?

Yesu anasema, “Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.” Marko 11:24. Kuna sharti kwa ahadi hii - kwamba tuombe sawasawa na Mapenzi ya Mungu. Lakini ni Mapenzi ya Mungu kutusafisha na dhambi zetu, kutufanya watoto Wake, na kutuwezesha kuishi maisha matakatifu. Hivyo tunaweza

kuomba baraka hizi, na kuamini kwamba tunazipokea, na kumshukuru Mungu kwamba tumepokea ahadi hizo.

Tangu sasa ninyi si mali yenu wenyewe; mmenunuliwa kwa bei kubwa. Kupitia tendo hili rahisi la kumwamini Mungu, Roho Mtakatifu amezaa maisha mapya ndani ya moyo wako. Wewe ni mtoto aliyezaliwa katika familia ya Mungu, na Yeye anakupenda kama vile anavyompenda Mwanawe.

Sasa kwa kuwa umejitoa kwa Yesu, usirudi nyuma tena, usijiondoe Kwake, lakini siku baada ya siku sema, "Mimi ni wa Kristo, nimejitoa Kwake," na umwombe Akupe Roho Wake ili Akutunze kwa neema Yake. Kama ilivyo, unapojitoa kwa Mungu, na kumwamini, basi, unakuwa mtoto Wake, ndivyo na wewe wanapaswa kuishi ndani Yake.

Hapa ndipo maelfu wanaposhindwa; hawaamini kwamba Yesu anasamehe kila nafsi, yaani mtu mmoja mmoja. Hawamtilii maanani Mungu katika Neno Lake. Ni fursa ya wote wanaotii masharti kujua wenyewe kwamba msamaha unatolewa kwa kila dhambi. Ondoa shaka kwamba ahadi za Mungu hazikukusudiwa kwa ajili yako. Ahadi za Mungu zipo kwa ajili ya kila nafsi inayotubu. Inueni macho juu, ninyi wenye mashaka na kutetemeka; kwa maana Yesu Yu hai ili atuombee. Mshukuruni Mungu kwa ajili ya zawadi ya Mwanawe mpendwa.

"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita; tazama, mambo yote yamekuwa mpya." 2 Wakorintho 5:17. Huenda mtu asiweze kutaja wakati au mahali hasa, au kufuatilia mlolongo wote kwamba mambo yalikuwaje katika huu mchakato wa uongofu; lakini hii haithibitishi kuwa wewe haujaongoka.

Mabadiliko yataonekana katika mwenendo, tabia, na utendaji wako. Tofauti itakuwa wazi na kuamuliwa kati ya vile ambavyo ulivyo sasa na ulivyokuwa. Nani ana moyo wako? Mawazo yetu yanamilikiwa na nani? Je, tunapenda kuzungumza juu ya nini au nani? Ni nani aliye na upendo wetu makini na nguvu zetu bora zaidi? Ikiwa sisi ni wa Kristo, mawazo yetu yapo pamoja Naye. Hakuna uthibitisho wa toba ya kweli isipokuwa inafanya kazi ya matengenezo.

Uzuri wa tabia ya Kristo utaonekana kwa wafuasi Wake. Ilikuwa furaha Yake Masihi kufanya Mapenzi ya Mungu. Kuna makosa mawili ambayo watoto wa Mungu hasa wanatakiwa kujilinda nayo: La kwanza ni lile la kujivunua kazi zao wenyewe, kujiamini kuwa wao wanaweza kufanya kitu fulani, ili kuweza kujileta wenyewe katika mapatano na Mungu. Yote ambayo mwanadamu anaweza kufanya bila Kristo yamechafuliwa na ubinafsi na dhambi. Ni neema ya Kristo pekee, kwa njia ya imani, ndiyo ambayo inaweza kutufanya watakatifu.

Kosa  la pili lililo kinyume na la hatari ni kwamba watu huamini kwamba imani katika Kristo huwaachilia wanadamu kutoka katika kuishika Sheria ya Mungu; kwamba kwa kuwa na imani pekee tunakuwa washiriki wa neema ya Kristo, matendo yetu hayana la kufanya katika suala la ukombozi wetu.

Utii ni tunda la imani. Haki inafafanuliwa kwa kiwango cha Sheria takatifu ya Mungu, kama inavyoonyeshwa katika zile Amri kumi (Kutoka 20:3-20). Kile kinachoitwa imani katika Kristo ambacho kinadai kuachilia watu kutoka katika wajibu wa utii kwa Mungu, sio imani, lakini ni kiburi na uelewa ulio na makosa. Sharti la uzima wa milele, kama lilivyo sasa ndivyo lilivyokuwa siku zote - kama ilivyokuwa katika edeni (au paradiso) kabla ya anguko la wazazi wetu wa kwanza, sharti hilo ni Utii mkamilifu kwa Sheria ya Mungu, ambayo ndiyo uadilifu mkamilifu.

Ikiwa uzima wa milele ungetolewa kwa sharti lolote pungufu ya hili, basi ni furaha ya sayari zote na mbingu imo hatarini. Njia ingelifunguliwa wazi kwa ajili ya dhambi, pamoja na msururu wake wote wa misiba na taabu, hata kama watu hawafi.

Kristo anabadilisha moyo. Anakaa moyoni mwetu kwa imani. Tunapaswa kudumisha uhusiano huu na Kristo kwa imani na kujitoa daima kwa mapenzi yetu Kwake; na mradi unafanya hivi, Yeye atafanya kazi ndani yake kutaka na kutenda kulingana na mapenzi Yake mema.

Kadiri unavyomkaribia Masihi, ndivyo utakavyoona ulivyo na

makosa zaidi machoni pako; maana maono yako yatakuwa wazi zaidi. Huu ni ushahidi kwamba udanganyifu wa Shetani unapoteza nguvu zake. Hakuna upendo wa kina kwa Yesu unaoweza kukaa katika moyo ambao hautambui dhambi yake wenyewe. Nafsi inayogeuzwa kwa neema ya Kristo itapendezwa na tabia Yake Mungu. Mtazamo wa dhambi zetu unasukuma na Yeye anayeweza kusamehe; na wakati nafsi, inatambua unyonge wake, na kumfikia Kristo, Yeye atajidhihirisha kwa uwezo Wake. Kadri hisia za kumhitaji zinavyotusukuma Kwake na kwa Neno la Mungu, ndivyo tutakavyokuwa na mitazamo iliyotukuka zaidi juu ya tabia Yake, na kwa ukamilifu zaidi tutaiakisi sura Yake.

Badiliko la mioyo ambalo kwalo tunafanyika kuwa wana wa Mungu linapatikana katika Biblia kama kuzaliwa. Tena linalinganishwa na kuota kwa mbegu nzuri iliyopandwa na mkulima. Ni Mungu Ndiye anayeleta chipukizi la majani kutokea na kisha ua, na mwishowe matunda. Ni kwa uwezo Wake mbegu hukua. Kama vile Ua linavyoligeukia jua, ili miale yake angavu isaidie katika ukamilifu mzuri na ulinganifu wake; ndivyo sisi tutakiwavyo kuligeukia Jua la Haki, ili nuru ya mbinguni iangaze juu yetu, ili tabia zetu ziweze kukuzwa katika kufanana na Kristo.

Je, unauliza, “Ninawezaje kukaa ndani ya Kristo?” Kama jinsi ulivyompokea Kristo hapo kwanza. "Basi kama mlimpokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika Yeye.” Wakolosai 2:6. Kwa imani wewe ukawa Wake Kristo; na kwa imani unapaswa kukua ndani Yake kwa kutoa na kupokea. Unapaswa kutoa yote, moyo wako, mapenzi yako, huduma yako, hebu jitoe Kwake ili kutii matakwa Yake yote; nawe sharti uvibebe vyote, yaani umchukue Kristo (Ambaye Ndiye vyote), Ambaye ni utimilifu wa baraka zote, Naye Akae moyoni mwako, Awe nguvu yako, Awe haki yako, na Msaidizi wako wa milele wa kukupa uwezo wa kutii.

Jiweke wakfu kwa Mungu asubuhi; fanya hii iwe kazi yako ya kwanza kabisa. Ombi lako liwe, Nitwae, Ee Bwana, niwe Wako kabisa. Ninaweka mipango yangu yote miguuni Pako. Nitumie leo katika

huduma Yako. Kaa nami, na kazi yangu yote na itimizwe ndani yako." Niepushe kuyafanya yale ambayo sipaswi kuyafanya, na kuyafanya yale ambayo napaswa kufanya. Hili ni jambo la kila siku. Kila asubuhi jiweke wakfu kwa Mungu kwa ajili ya siku hiyo. Peleka mipango yako yote Kwake, ili itekelezwe au iache kutokana na majaliwa Yake yatakavyoonyesha. Hivyo siku baada ya siku unaweza kuendelea ku yatoa maisha yako mikononi mwa Mungu, na hivyo maisha yako yatafinyangwa zaidi na zaidi kufanana na maisha ya Kristo.

Maisha ndani ya Kristo ni maisha ya utulivu. Kunaweza kuwa hakuna furaha yenye mihemko ya hisia, lakini kunapaswa kuwa na uvumilivu wa kuendelea kudumu katika Imani yenye matumaini. Wakati akili inapokaa juu ya ubinafsi, inageuzwa mbali na Kristo, Aliye chanzo cha nguvu na uhai. Kwa hivyo, ni juhudi ya mara kwa mara ya Shetani kutoa usikivu kutoka kwa Mwokozi na hivyo kuzuia muungano na ushirika wa roho na Kristo.

Kristo alipotwaa asili ya mwanadamu juu Yake, Aliufungamanisha ubinadamu Kwake kwa kifungo cha upendo ambacho hakiwezi kamwe kuvunjwa na mamlaka yoyote, isipokuwa chaguo la mwanadamu mwenyewe. Shetani ataendelea kuweka vivutio vya kutushawishi kuvunja uhusiano huu yaani kuchagua kujitenga na Kristo. Lakini wacha tuendelee kuinua macho yetu kumtazama Kristo, Naye atatuhifadhi. Tukimtazama Masihi, tuko salama. Hakuna kinachoweza kutung'oa kutoka mkononi Mwake. Yote ambayo Kristo alikuwa kwa wanafunzi, anatamani yawe kwa watoto Wake leo.

Yesu alituombea, na aliomba kwamba tuwe na umoja Naye, kama vile Yeye alivyo mmoja na Baba. Huu ni muungano wa thamani kiasi gani! Hivyo, tukimpenda na kukaa ndani Yake, "Tutakua hata tumfikie Yeye katika yote, Yeye Aliye kichwa, Kristo." Waefeso 4:15.

Mungu Ndiye chanzo cha uhai na nuru na furaha kwa ulimwengu. Popote uzima wa Mungu unapokuwepo ndani ya mioyo ya watu, uzima huo utatiririka kwa wengine kwa upendo na baraka.

Furaha ya Mwokozi wetu ilikuwa katika kuinuliwa na ukombozi wa wanadamu walioanguka. Kwa hili hakuyahesabu maisha Yake kuwa ya thamani Kwake Yeye Mwenyewe, bali aliustahimili msalaba na kuidharau aibu. Wakati upendo wa Kristo umo ndani ya moyo, ni kama manukato au harufu nzuri isiyoweza kufichwa. Upendo kwa Yesu utadhihirika katika hamu ya kufanya kazi kama Yeye alivyofanya kazi kwa ajili ya baraka na kuinuliwa kwa ubinadamu. Upendo kwa Kristo huleta mwitikio wa upendo, rehema, na huruma yenye mguso kwa viumbe vyote ambavyo Baba yetu wa mbinguni Anavitunza. Wale walio washiriki wa neema ya Kristo watakuwa tayari kutoa dhabihu yoyote, ili wengine aliowafia wapate kushiriki zawadi ya mbinguni. Watafanya yote wawezayo kufanya duniani, ili dunia iwe mahali bora zaidi katika kukaa kwao humo. Roho hii ndiyo chanzo cha uhakika cha nafsi iliyoongoka kweli kweli. Mara tu mtu anapokuja kwa Kristo ndipo unazaliwa ndani ya moyo wake, hamu ya kufanya Kristo ajulikane kwa wengine na kwamba ni urafiki wa thamani gani ameupata kwa Yesu (In Jesus I found a friend). Ikiwa tumeonja na kuona kwamba Bwana ni mwema, tutakuwa na kitu cha kusema. Tutajaribu kuwasilisha kwa wengine vivutio vya Kristo na mambo yasiyoonekana ya ulimwengu ujao. Kutakuwa na nguvu yenye matamanio makubwa katika kufuata njia ambayo Yesu aliipita.

Na jitihada za kuwabariki wengine zitaleta mwitikio wa baraka juu yetu wenyewe. Wale ambao wanakuwa washiriki katika kazi ya upendo, huletwa karibu zaidi na Muumba wao. Roho ya kufanya kazi bila ubinafsi kwa ajili ya wengine hutoa kina, uthabiti, na kuwa na tabia ya kupendeza kama Kristo kwa mhusika, na kisha huleta amani na furaha kwa mhusika (mtoaji). Nguvu huja kwa kujizoeza. Hatuhitaji kwenda katika nchi za kipagani, au hata kuacha mazingira ya nyumba zetu, ikiwa hapo ni pale ambapo wajibu wetu uko, ili kufanya kazi kwa ajili ya Kristo. Kwa roho ya upendo tunaweza kufanya kazi kwa unyenyekevu katika maisha “kwa Bwana.” Wakolosai 3:23. Ikiwa upendo wa Mungu umo moyoni, utadhihirika katika maisha yetu. Haupaswi kungojea hafla nzuri au kutarajia uwezo wa ajabu kabla ya kwenda kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. Wanafunzi wanyenyekevu na

maskini zaidi wa Yesu wanaweza kuwa baraka kwa wengine wakati wote.

Kuna njia nyingi ambazo Mungu anatafuta kujitambulisha kwetu na kutuleta katika ushirika pamoja Naye. Ikiwa tutasikiliza tu, Asili huzungumza na hisia zetu bila kukoma. Kazi zilizoumbwa na Mungu zitatufundisha masomo ya thamani ya utii na uaminifu.

Hakuna machozi yanayotolewa ambayo Mungu hayatambui. Hakuna mwenendo asioutia alama. Kama tungeweza kumwamini kikamilifu, mahangaiko yote yasiyofaa yangetupiliwa mbali. Maisha yetu yasingejazwa na kukata tamaa kama ilivyo sasa; kwa maana kila kitu, kiwe kikubwa ama kidogo, kingeachwa mikononi mwa Mungu.

Mungu huzungumza nasi kupitia kazi Zake na majaliwa na kupitia ushawishi wa Roho Wake juu ya moyo yetu. Mungu anazungumza nasi katika Neno Lake. Hapa tunayo mistari iliyo wazi zaidi ya ufunuo wa tabia Yake, kushughulika Kwake na wanadamu, na kazi kuu ya ukombozi. Jaza moyo wote kwa Neno la Mungu. Neno ni maji yaliyo hai, yakizima kiu yako iwakayo. Neno ni mkate wa uzima kutoka mbinguni.

Siri ya ukombozi ni jambo ambalo malaika wanatamani kuliangalia na kulijua ila ni fumbo na siri; ukombozi wa mwanadamu itakuwa ndiyo sayansi na wimbo wa waliokombolewa katika enzi zote zisizo na kikomo za milele. Kama ni hivyo, Je, haifai basi tufikirie sasa kwa makini na kujifunza leo hii? Tunapotafakari juu ya Mwokozi, kutakuwa na njaa na kiu ya nafsi ya kuwa kama Yeye Ambaye tunamwabudu.

Biblia iliandikwa kwa ajili ya watu wa kawaida. Kweli kuu zinazohitajika kwa wokovu zinafanywa wazi kama mchana. Hakuna kitu kinachohesabiwa kuimarisha akili kuliko kujifunza Maandiko Matakatifu. Lakini kuna faida kidogo inayopatikana kwa kusoma Biblia haraka-haraka. Fungu moja likisomwa kwa makini hadi tukagundua umuhimu kwa akili zetu na uhusiano wake, na mpango wa wokovu ukawa dhahiri, huu ndio usomaji wa thamani zaidi kuliko usomaji wa sura nyingi bila malengo dhahiri na hakuna maagizo

chanya yaliyopatikana.

Weka Biblia yako pamoja nawe. Upatapo nafasi, isome; yaweke maandishi kwenye kumbukumbu yako. Hatuwezi kupata hekima bila uangalifu wa dhati na kujifunza kwa sala.

Kamwe Biblia haipaswi kusomwa bila maombi. Kabla ya kufungua kurasa Zake, tunapaswa kuomba nuru ya Roho Mtakatifu, nayo itatolewa. Malaika kutoka katika ulimwengu wa nuru watakuwa pamoja na wale ambao kwa unyenyekevu wa moyo wanatafuta mwongozo wa Mwenyezi Mungu. Je, ni kwa jinsi gani Mungu anawathaminiwanadamu? Yeye alimtoa Mwanawe ili afe kwa ajili yao na anamtuma Roho Wake Mtakatifu kuwa mwalimu wa mwanadamu, Naye ni kiongozi wa kudumu!

Kupitia asili na ufunuo, kupitia majaliwa Yake, na kwa ushawishi wa Roho Wake, Mungu anazungumza nasi. Lakini haya hayatoshi; tunahitaji pia kumimina mioyo yetu Kwake. Ili kuwasiliana na Mungu, sharti tuwe na kitu cha kumwambia kuhusu maisha yetu halisi, maisha ya kila siku. Maombi ni kufungua moyo kwa Mungu kama kwa rafiki. Sio kwamba ni sharti tumjulishe Mungu mambo yalivyo kwetu, bali ni ili Atuwezeshe kumpokea Yeye mioyoni mwetu. Maombi hayamshushi Mungu kwetu, lakini maombi hutupeleka juu Kwake.

Baba yetu wa mbinguni anasubiri kutupa utimilifu wa baraka Zake. Inashangaza kiasi gani kwamba sisi tunaomba kidogo sana! Mungu Yuko tayari kutubariki na Anawiwa kusikia maombi ya dhati ya watoto Wake walio wanyenyekevu zaidi. Malaika wa mbinguni wanashangaa wanapofikiria juu ya wanadamu maskini wasiojiweza, ambao wako chini ya majaribu, nao wanaomba kidogo sana na wana imani ndogo sana, wakati Moyo wa Mungu wenye upendo usio na kikomo una matamanio nao, Naye Yupo tayari kuwapa zaidi ya vile wanavyoweza kuomba au kufikiria.

Giza la mwovu linawafunika wale wanaopuuza kuomba. Majaribu ya kunong'ona ya adui huwashawishi wanadamu kutenda dhambi; na

yote ni kwa sababu hawatumii fursa ya maombi. Walakini maombi ndio ufunguo katika mkono wa imani kufungua ghala ya mbinguni, ambapo rasilimali zisizo na kikomo za Mweza wa yote zinatunzwa.

Kuna masharti fulani ambayo kwayo tunaweza kutarajia kwamba Mungu atasikia na kujibu maombi yetu: Moja ni kwamba tunahisi hitaji letu la msaada kutoka Kwake. Tukiwaza maovu mioyoni mwetu, tukishikamana na dhambi yoyote tuijuayo; Bwana hatatusikia; lakini sala ya mtu aliyetubu na aliyeungama hukubaliwa daima. Wakati wote makosa yanayojulikana yanaposahihishwa, tunaweza kuamini kwamba Mungu atajibu maombi yetu.

Kipengele kingine cha maombi yenye nguvu ni imani. Wakati maombi yetu yanaonekana kutojibiwa, tunapaswa kushikilia kwa bidii ahadi Zake; kwani wakati wa kujibiwa utakuja hakika, na tutapokea baraka tunazozihitaji zaidi. Lakini kudai kwamba maombi daima yatajibiwa kwa namna tutakavyo na kila kitu tunachokitamani ni dhana za kufikirika.

Tunapokuja kwa Mungu katika maombi, tunapaswa kuwa na roho ya upendo na msamaha ndani ya mioyo yetu wenyewe. Kuendelea kudumu katika maombi kumefanywa kuwa sharti la kupokea majibu yetu. Sharti tuombe kila wakati ikiwa tunataka kukua katika imani na uzoefu.

Tunapaswa kuomba katika mzunguko wa familia, na zaidi ya yote hatupaswi kupuuza maombi ya siri, kwa maana haya ndiyo maisha ya kiroho. Sala ya familia au ya hadhara pekee yake haitoshi. Maombi ya siri yanasikika kwa Mungu Ajibuye maombi.

Hakuna wakati au mahali pasipofaa kutoa ombi kwa Mungu. Katika umati wa watu mtaani, katikati ya shughuli za kibiashara, tunaweza kutuma ombi kwa Mungu na kumsihi Mungu Atupe mwongozo wa Kiungu.

Hebu roho na ivutwe na kwenda juu, ili Mungu atupe pumzi ya anga

la mbinguni. Sisi tunaweza kuwa karibu sana na Mungu kiasi kwamba katika kila jaribu lisilotarajiwa mawazo yetu yatamgeukia Yeye kwa ile kawaida ya ua linavyoligeukia jua. Weka mahitaji yako, furaha yako, huzuni zako, wasiwasi wako, na hofu zako mbele za Mungu.

Wewe huwezi kumlemea; huwezi kumchosha. Yeye hachoshwi na matakwa ya watoto Wake.

Tunapata hasara tunapopuuza fursa ya kujumuika pamoja ili kuimarishana na kutiana moyo sisi kwa sisi katika utumishi kwa Mungu. Ikiwa Wakristo watashirikiana pamoja, wakisemezana kuhusu upendo wa Mungu na Kweli za thamani za ukombozi, mioyo yao wenyewe ingeburudishwa na wangeburudishana wao kwa wao.

Ni sharti tukusanyike pamoja kwa ajili ya msalaba. Kristo na Yeye aliyesulubiwa vinapaswa kuwa mada ya kutafakari, mada ya mazungumzo, na hisia zetu za furaha zaidi. Tunapaswa kuweka katika mawazo yetu kila baraka tunayoipokea kutoka kwa Mungu, na tunapotambua upendo Wake mkuu tunapaswa kuwa tayari kuamini kila kitu kilicho katika mikono ile iliyotundikwa msalabani kwa ajili yetu.

Nafsi inaweza kupaa karibu na mbingu kwa mbawa za sifa kwa Mungu. Tunapoonyesha shukrani zetu, ndivyo tukaribiavyo kuabudu na majeshi ya mbinguni. Wengi nyakati fulani wanatatizwa na mapendekezo ya kutilia shaka kuhusu Mungu. Mungu kamwe hatuambii tuamini bila kutoa uthibitisho wa kutosha wa kujenga imani yetu. Tunaweza kuficha uhalisia au ukweli Kwa namna tuwezavyo, ila sababu halisi ya shaka na kutokuamini, katika hali nyingi, ni kupenda dhambi. Ni sharti tuwe na nia ya dhati ya kujua Ukweli na utayari wa moyo kuitii.

Kabla ya kuingia kwa dhambi, Adamu alifurahia ushirika wa wazi na Muumba wake; lakini tangu mwanadamu alipojitenga yeye mwenyewe kutoka kwa Mungu kwa kutenda dhambi, jamii ya kibinadamu imekatiliwa mbali na upendeleo huu mkuu. Kwa mpango wa

ukombozi, hata hivyo, njia imefunguliwa ambayo kwayo wakaaji wa dunia wanaweza bado kuwa na uhusiano na Mbingu. Mungu amewasiliana na wanadamu kwa Roho Wake, na nuru ya Bwana imekuwa ikipandikizwa ulimwenguni kwa mafunuo, kupitia watumishi Wake wateule. “Watu watakatifu wa Mungu walinena kama walivyokuwa wakiongozwa na Roho Mtakatifu.” 2 Petro 1:21.

Wakati wa karne ishirini na tano za kwanza za historia ya mwanadamu, hapakuwa na ufunuo ulioandikwa (Musa aliishi miaka 2500 hivi baada ya Adamu kuumbwa, na ndiye mwandishi wa kwanza). Wale ambao walikuwa wamefundishwa na Mungu, waliwasilisha ujuzi wao kwa wengine, na maarifa haya yalipitishwa kutoka kwa baba kwenda kwa mwana, kupitia vizazi vilivyofuatana. Maandalizi ya Neno lililoandikwa yalianza wakati wa Musa.

Mafunuo yaliyovuviwa yalijumuishwa katika kitabu kilichovuviwa. Kazi hii iliendelea kwa muda mrefu kipindi cha miaka elfu na mia sita (1600), kutoka kwa Musa, mwanahistoria wa uumbaji na Sheria, hadi Yohana, mwandishi wa Kweli kuu za injili (takribani Kutoka 1500 KK hadi 100 BK).

Biblia inaelekeza kwa Mungu kama mwandishi Wake; lakini iliandikwa kwa mikono ya wanadamu; na kwa mtindo wake tofauti vitabu vyake mbalimbali vinawasilisha sifa za waandishi kadhaa. Kweli zilizofunuliwa zote “hutolewa kwa pumzi ya Mungu” (2 Timotheo 3:16); lakini zinaonyeshwa kwa maneno ya wanadamu, kwani si imla, ila walipewa njozi na ndoto na wakaandika kwa maneno yao. Roho Mtakatifu ametoa nuru katika akili na mioyo ya watumishi Wake. Amewapa ndoto na maono, alama na takwimu; na wale waliofunuliwa Kweli hizi, wameonyesha wenyewe mawazo hayo katika lugha ya kibinadamu.

Amri kumi zilinenwa na Mungu Mwenyewe, na ziliandikwa kwa mkono Wake Mwenyewe. Amri Kumi ni za Mungu Mwenyewe. Tunatakiwa tuwe waangalifu sana, kwani amri za mataifa yetu tunazitilia maanani, na tunapozivunja tunapata shida, sembuse Amri

za Mwenyezi Mungu? Hakuna awezaye kushika sheria na kutembea na Mwenyezi Mungu isipokuwa amepata msaada kutoka Kwake, na Kila mwanadamu aombaye msaada huo, Mungu Yupo tayari kumpa.



SOMA AHADI ZA MUNGU NA KUZIDAI ILI USIWE NA UTUPU MOYONI NA KUFIKIRIA KWAMBA UMEPUNGUKIWA NA KITU, NA ULE UPUNGUFU UTAJAZWA KWA FASHENI AU KUJIONYESHA.

Kusali ni sisi tunazungumza na Mungu, na Kusoma Biblia ni Mungu anazungumza na sisi! Je, ipi ni muhimu zaidi? Yote ni muhimu katika Mawasiliano, ila kwa akili yangu, Maneno ya Mungu ndiyo mazito na muhimu kuliko maneno yangu! George Muller aliye na visa vingi vya kustajaabisha, ambaye tunataka kutafsiri Biografia yake, alisema kwamba kati ya Mafungu ya Biblia 31,102 kuna Ahadi 30,000! Yawezekana ni kweli japokuwa Hakika hizo ni nyingi sana. Mtu huyu wa Mungu alikuwa na watoto yatima 10,000 Uingereza na akawalisha, na kuwavisha na kuwasomesha, akitegemea hizi ahadi za Mungu. Katika mazishi yake, walileta shajara zake 50 ambazo alikuwa ameziandika kwa miaka 50, na humo walikuta zaidi ya maombi 50,000 yaliyojibiwa! Anza kuandika mambo kwenye shajara utashangaa!

Wakati mwingine kujua nini ni ahadi inakuwa ngumu, na inategemeana na jinsi unavyosoma! Mungu amesema zaidi ya mara 2300 na imeandikwa “Bwana akasema” “Kama asemavyo Bwana” “Bwana akamwambia” nk. Kwenye kitabu cha Walawi, Mwenyezi Mungu anasema au anatamka maagizo kuliko mahali pengine popote! Mimi nayachukulia Maagizo Yake yote kama ahadi! Maana yasipofanywa kuna kitu kitatokea! Mfano KumbuKumbu la Torati 28 ina ahadi 126 na Walawi 26 ambayo inafanana nayo, ina ahadi 85 hivi, na kisha Zaburi 37 ina ahadi 25 hivi. Zaburi 23 ambayo ni maarufu, kila mstari wake ni ahadi isipokuwa mstari mmoja tu, angalia ni upi! Ahadi ambazo ni hasi ni ahadi, maana ukifanya kinyume utabarikiwa mfano angalia katika Kumbukumbu la Torati 28, hizi ahadi hasi ni ahadi! Yaani tutakaposhika Amri Zake, hatutalaniwa shambani au mjini, kapu letu la kukandia litabarikiwa, uzao wetu na uzao wa wanyama

utabarikiwa, hatutapata mashaka na kukemewa…………….etc

"15 Lakini itakuwa usipotaka kuisikiza sauti ya Bwana, Mungu wako, usiyaangalie kufanya maagizo Yake yote na amri Zake, nikuagizazo hivi leo, ndipo zitakapokujia laana hizi zote na kukupata.
16 Utalaaniwa mjini, utalaaniwa na mashambani.
17 Litalaaniwa kapu lako na chombo chako cha kukandia.
18 Utalaaniwa uzao wa tumbo lako, na uzao wa nchi yako, maongeo ya ng'ombe wako, na wadogo wa kondoo zako.
19 Utalaaniwa uingiapo, utalaaniwa na utokapo,
20 Bwana atakuletea laana na mashaka, na kukemewa, katika yote utakayotia mkono wako kuyafanya, hata uangamie na kupotea kwa upesi; kwa ule uovu wa matendo yako, uliyoniacha kwayo.
21 Bwana atakuambatanisha na tauni, hata atakapokwisha kukuondoa katika nchi uingiayo kwa kuimiliki "

Kwa maneno mengine kila Neno la Mungu linapotamka kitu, na tusilifuate, basi hayo Maneno yanaambatana na laana! Na kwanini tupate laana wakati Mungu anataka kutubariki?  Mfano maagizo ya kujenga Patakatifu au hekalu aliyotoa Mungu kwa Injinia na disaina Bezaleli na Aholiabu, unafikiri nini kingetoa endapo wasingefuata Maneno kama ya Kutoka 25-31? Angalia Kutoka 27 "Nawe fanya madhabahu ya mti wa mshita; urefu wake utakuwa ni dhiraa tano, na upana wake dhiraa tano; hiyo madhabahu itakuwa mraba; na kwenda juu kwake kutakuwa dhiraa tatu.
2 Nawe fanya pembe nne katika pembe zake nne; hizo pembe zitakuwa za kitu kimoja na madhabahu; nawe utayafunika shaba."
3 Na vyombo vyake vya kuyaondoa majivu yake utavifanya, na majembe yake, na mabakuli yake, na uma zake, na meko yake; vyombo vyake vyote utavifanya vya shaba. "

Unafikiri nini kingetokea kama wasingelifuata maagizo?  Kitabu cha Mithali pia watu wengi wamesema hizo sio ahadi ila ni kanuni, ila ni vigumu kutofautisha ahadi na kanuni mfano

*Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee.

Au

*Mguu wako usiingie katika nyumba ya jirani yako ila kwa kiasi; Asije akakukinai na kukuchukia.  Au

*Aibaye mali ya babaye au mamaye, na kusema, Si kosa; Mwana huyo ni rafiki wa mtu mharibifu.

Je hizi ni ahadi? Mimi nimechukulia nyingi kama ahadi!

Tunapoomba tumrudishie Mungu Maneno Yake! Tuombee Nini? Kila ahadi ya Mungu ni jambo la kuombea! Tumeona tuweze kuziwekea rangi ahadi hizi, ili tuwe na umakini wa kuziangalia na kuziomba au kuzidai, maana Mungu Mwenyewe amesema tumsumbue, tuinuke, tusibweteke au kuchoka! Maana kwenye pambano kuu adui aweza kusema kwamba Mungu analazimisha hizi baraka kwetu kutununua, na wala hatujaomba hayo mambo. Hata hivyo tunaambiwa hatupewi, kwa vile hatuombi! Mimi na wewe hatutakosa kwa vile tutaziomba hizi ahadi.

Kama wazazi wetu ambao ni wanadamu tu, hutunza ahadi zao, sembuse Baba wa Mbinguni? Kuna huduma hapa wamehesabu ahadi za Mungu za moja kwa moja kuwa 8100, niliwaita kuwaomba wakasema nitoe dola 400. nikaona bora kujitafutia mwenyewe na kuzisoma! Vitabu vyenye ahadi nyingi ni Yeremia, Isaya na Ezekieli, kila kimoja kina zaidi ya ahadi 1000, na hivyo vikijumuishwa hivi vitatu vina ahadi zaidi ya 3000!

Ahadi za Mungu ni mbegu, ni tumaini, ni upendo ni hakikisho. Hazitumiki hapa na pale tu, bali daima kutubadilisha katika maisha. Ni daraja la kututoa kwenye utumwa wa maisha yetu mabaya ya zamani na kuwa wapya katika Bwana. Mungu ana uwezo wote, maarifa yote, na Yupo kila mahali. Anatuita kupata utukufu na mema Yake, na kwa nguvu hii ametupa ahadi zenye thamani na za ajabu. Tukijaza akili zetu na hizi ahadi, Yeye hutupa amani moyoni, mahitaji na zaidi ya hayo. Macho yetu hufunguka kwa yote yawezekanayo/possibilities. Tunapata ujasiri wa kukumbana na changamoto za maisha.

Hebu ahadi za Mungu zikukumbushe haya unapozisoma

1. Upendo Wake kwako-usimtilie mashaka Mungu. Jua Yeye anakupenda kuliko unavyojipenda, na anakutakia mema kuliko wewe mwenyewe. Yeye ni Mungu wa rehema, upendo na haki, hata kwenye majanga, tutashangaa kwamba kila kitu aliruhusu kufanyika kwaajili ya mema kwetu katika dunia yetu yenye mapambano na adui. Kama Mungu anaangalia ndege wadogo na kuwatunza, sisi je?

2. Hebu tuangalie upendo wa Mungu na siyo ukubwa wa matatizo yetu, na tuache ahadi kupanua njozi Mungu aliyonayo kwetu. Ahadi za Mungu ni kama mawani yanasohahisha uoni potofu! Hakuna kitakachotutenganisha na upendo wa Mungu, kamwe!

Soma Warumi 8

35 Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! Ni dhiki au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga?.
37 Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda.
38 Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo,
39 wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.

Tukiishi kwa kumtegemea Yeye, hakuna tutakachotupiwa na maisha ambacho kitakuja kati yetu Naye~Tutajua anatupenda na anajali sana!

3. Hebu ahadi za Mungu ziwe dawa na tiba kwa nguvu ya kufa moyo na mawazo hasi. Wengi tuna tabia ya kutegemea mambo kuwa mabaya kuliko yalivyo- Soma Waefeso 3:20

20 Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu;

4.Hebu ahadi za Mungu zikusaidie mwitikio wako kwa yote yale yanayohusu Imani. Tunapopata msongo tunapotea uoni wa uwezekano wa kutatua shida na upendo wa Mungu. Ahadi Zake Bwana zinatuonyesha kwamba Yeye ana uwezo wote na atafanya mambo kuliko tunavyofikiri.

*Walawi 26:8* Na watu watano wa kwenu watawafukuza watu mia, na watu mia wa kwenu watawafukuza watu elfu kumi; na adui zenu wataanguka mbele yenu kwa upanga.

Wafilipi 4:*13* Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.

Nguvu ya Ahadi iko ndani ya tabia ya Mungu na nguvu ya Neno Lake. Tunapopanda mbegu za ahadi za Mungu katika mioyo yetu, basi zitatoa matunda na kutulisha wakati wa changamoto za maisha.

Japokuwa ahadi zingine hazijawekwa humu, maombi yangu ni kwamba utaendelea kuzitafuta katika ahadi, Neno, shuhuda, maagizo, amri, mausia ya Mungu kama ambavyo Zaburi 119 inavyoshauri katika mashairi yake nane. Hebu hizi ahadi za

thamani, kupita zote duniani zinyweshee imani yako, zifanye moyo wako kuwa mpya, na kukufanya uongozwe kuishi maisha yale ambayo, Mwenyezi Mungu anataka uishi kwaajili Yake.

Ukigundua ahadi zingine, tuandikie ili tuendelee kuzikusanya!

Mwaka wa heri!

Enendeni Mtandaoni Kote Ministry

Grace Momadi Masaka

Huduma kwa Ughaibuni Uhamishoni Mtandaoni na Majumbani

Na Roho na Bibi-arusi wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, Njoo! Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure

Yeye Mwenye kuyashuhudia haya asema, Naam; Naja upesi. Amina; na uje, Bwana Yesu. Neema ya Bwana Yesu na iwe pamoja nanyi nyote. Amina.

Maranatha